# Nipashe

Jumamosi Aprili 4, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580197

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Mahakama yataifisha bil. 16.7/- za upatu toka kampuni ya kigeni

UKURASA 2




UKURASA 13

TISHIO CORONA

# Waziri aagiza msako waendesha twisheni

**ASEMA** wanakiuka amri ya serikali, Mbunge ataka ulinzi walioko karantini, mgonjwa mwingine apona, Masanja Mkandamizaji matatani... *Endelea ukurasa 2, 3, 7, 8*



Baadhi ya wateja wanaohitaji kuingia katika soko la Makoroboi, jijini Mwanza, wakinawa mikono kwa wakati mmoja, kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, jana, jambo ambalo si zuri kwa usalama wao. **PICHA: NEEMA EMANUEL**



## BAA LA CORONA

PAMOJA na serikali kufunga shule kutokana na tishio la corona, watoto wengi wameonekana kuzurura, huku wengine wakitumikishwa sokoni. Hali hii ni hatari kwani inaweza kuchangia kuenea kwa maradhi ya corona ambayo ni tishio duniani. Katika kujikinga na corona;

* Epuka mikusanyiko ya watu
* Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
* Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
* Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo.

## AFARIKI KWA KUJINYONGA BAADA YA MTOTO KUFA

UKURASA 3

# Watoto warandaranda mitaani na kuibua hofu

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



MICHEZO SIMBA YAIKEBEHI YANGA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Ndalichako aagiza kukamatwa walimu wanaofundisha twisheni

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Elimu, Sanyansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amewaagiza wakurugenzi, wakuu wa wilaya na mikoa kuwachukulia hatua wale wote walioanzisha vituo vya mafunzo ya ziada (tuition) wakati ambao shule zote zimefungwa kwa ajili ya kujikinga na corona.

Profesa Ndalichako alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma na kuwataka wanafunzi walioko nyumbani kuacha kuzurura ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

"Wanafunzi watambue kuwa hiyo si likizo bali wamerudi nyumbani kwa sababu ya janga kubwa linaloitesa dunia la virusi vya corona. Kuna baadhi ya sehemu baada ya kusikia watoto wako nyumbani wameanzisha 'tuition'. Nawataka wote walioanzisha 'tuition' waache mara moja," alionya.

Ndalichako alitoa maelekezo kwa wakurugenzi, wakuu wa wilaya na mikoa, wasimamie kikamilifu maelekezo ya serikali na kutowafumbia macho watu walioanzisha vituo vya kufundishia kwa sababu wanapingana na maelekezo na wanakuwa tishio la usalama katika maeneo hayo.

Kadhalika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Misaada kwa Watoto (Unicef), wametoa angalizo na tahadhari ambazo watoto, wazazi, walezi na walimu wanapaswa kuzichukua wakati wote wa likizo.

"Kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona, walimu wakuu wasiwaruhusu wanafunzi kukusanyika katika maeneo shule kwa kipindi chote ambacho shule zimefungwa," tangazo lilielekeza hivyo.

Tahadhari nyingine iliyotolewa, inaitaka jamii iwalinde wanafunzi na watoto wote katika maeneo yao kwa kuhakikisha hawaendi katika maeneo hatarishi yakiwamo yenye msongamano.

Kadhalika wametahadharisha wazazi na walezi wazungumze na watoto wao kuhusu njia za kujikinga na virusi vya corona na kuwasaidia kuendelea kujisomea wakiwa nyumbani.



Wananchi wakitembea kwa miguu katika eneo la Jangwani, wakielekea katikati ya Jiji la Dar es Salaam jana, kutokana na shida ya usafiri iliyosababishwa na mabasi ya daladala kupakia abiria wanaotosha kwenye viti, kutekeleza agizo la serikali kama tahadhari ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mahakama yataifisha bil. 16.7/- za upatu toka kampuni ya kigeni

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa, imetaifisha Sh. bilioni 16.7 za upatu zilizokuwa zikimilikiwa isivyo halali na Kampuni ya IMS Marketing Tanzania Limited kuwa mali ya serikali.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), kuomba fedha hizo ambazo zilipatikana kwa njia ya upatu zitaifishwe.

Hata hivyo, mahakama hiyo imekataa ombi la DPP la kuitaka itoe amri ya kuiamuru Benki ya Afrika (BOA), kulipa riba ya kipindi chote walichohifadhi fedha hizo.

Uamuzi huo ulisomwa na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Elinaza Luvanda, baada ya kusikiliza maombi ya DPP yaliyowasilishwa chini ya kiapo cha Wakili wa Serikali, Esterzia Wilson na Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Fadhili. Jopo la Mawakili wa Serikali liliongozwa na DPP akisaidiana na Mawakili wa Serikali Wakuu, Shadrack Kimaro na Christopher Msigwa.

Walalamikiwa katoka maombi ya msingi, Rais wa Ujerumani Manon Huebenthal, Rais wa Uingereza, Frank Rickeltis na Kampuni ya IMS Marketing Tanzania Ltd.

Akisoma uamuzi huo jana, Jaji Luvanda alisema DPP aliwasilisha maombi ya kutaka mahakama itaifishe mali ambazo ni Dola za Marekani 1,351,597.79 na Euro 5,377,306.56, zote mbili zikiwa kwa jina la IMS Marketing Tanzania Limited zilizofunguliwa katika benki ya BOA.

Alisema mali hizo zilitokana na biashara ya upatu licha ya kwamba kampuni hiyo ilisajiliwa kwa shughuli za masoko.

Jaji Luvanda alisema DPP aliwasilisha maombi hayo yaliyoungwa mkono na hati mbili za viapo zilizowasilishwa na Wakili wa Serikali, Estazia Wilson na Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Fadhili, wakielezea jinsi washitakiwa hao walivyohusika katika kutenda uhalifu wa kuendesha mpango wa upatu na utakatishaji fedha.

Alisema wadaiwa waliitwa kwa kupitia matangazo mbalimbali na hawakuthubutu kuwasilisha kiapo kinzani na kwamba kesi ilipofunguliwa Mahakama ya Kisutu zilitolewa hati za kukamata lakini walikuwa mafichoni.

"Katika hali hii wajibu maombi hawakukana hati ya kiapo hivyo waleta maombi wamethibitisha maombi yao na fedha zinataifishwa kuwa mali ya serikali," alisema Jaji Luvanda.

Hata hivyo, alisema anakataa ombi la DPP la kutaka mahakama itoe amri ya kuamrisha BOA kulipa riba ya kipindi chote walichohifadhi fedha hizo lakini anakubaliana na mahakama kutoa nafuu nyingine na kwamba riba ilitakiwa kuingia katika eneo hilo.

"Kiasi cha riba hakikuelezwa kwenye hati ya kiapo na watu wa benki ya BOA si wadaiwa katika maombi hayo na hawakuitwa kujitetea, hivyo nikitoa amri dhidi yao kwa maoni yangu ni kukiuka haki yao ya kusikilizwa," alisema.

Aliongeza kuwa haikuelezwa namna benki hiyo ingenufaika na fedha hizo walizohifadhi, hivyo, alishauri waleta maombi kutafuta njia nyingine ya kuwasilisha ombi kuhusu riba.

DPP Biswalo Mganga akisaidiana na Kimaro na Msigwa. waliomba amri ya kutaifisha fedha hizo ili kuzuia wahalifu kufaidika na makosa ya jinai waliyotenda.

DPP pia iliomba Mahakama kuiagiza Benki ya BOA Limited, kulipa riba kwa kukaa na kiasi hicho kikubwa cha fedha tangu Januari 19, 2018, wakati wakijua fedha hizo sio halali.

DPP Mganga alidai Januari 19, 2014, raia hao wa kigeni walikuja nchini Tanzania na kusajili IMS Marketing Tanzania Limited, kampuni ambayo ilipewa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni leseni ya kutoa huduma mbalimbali za masoko.

Ilidaiwa kuwa ukusanyaji wa fedha kutoka kwa umma na kuendesha upatu kwa ujumla haikuwa miongoni mwa malengo ya biashara ambayo kampuni hiyo iliendesha.

Katika tarehe tofauti, washitakiwa hao wawili walifungua akaunti tajwa katika benki hiyo baada ya kusajili kampuni, ambayo ina uhusiano wa karibu na kampuni nyingine ya IMS International Marketing Services ya Singapore.

Kampuni hiyo ya Singapore ina uhusiano wa karibu na ni sehemu ya operesheni ya kampuni ya Onecoin Limited, iliyoanzishwa Aprili 2014 huko Gibraltar na ina ofisi nchini Bulgaria, Falme za Kiarabu.

Waliieleza mahakama kwamba, shughuli za kampuni ya Onecoin Limited na kampuni tanzu katika mamlaka mbalimbali zilisimamishwa na akaunti zao za benki kufungwa kwa sababu ya kujihusisha na utakatishaji fedha uliosababishwa na mchezo haramu wa upatu.

Kutokana na kusimamishwa kwa shughuli hizo, Onecoin Limited ilitangaza kwenye akaunti yake ya facebook na wavuti zake kwamba wanachama wanapaswa kulipa vifurushi na michango yao kupitia akaunti za benki zilizopo katika Benki ya BOA.

Kwa tarehe tofauti, jumla ya 16, 720, 858, 579. 47 zilipokelewa kutoka kwenye akaunti zote tatu za benki. Kiasi hicho kinajumuisha jumla ya Dola za Marekani 1,351,597.79 katika akaunti mbili za USD na zingine za Euro 5,377,306.56 katika akaunti ya Euro.

Kuzingatia ushahidi huo, DPP alifungua kesi ya uhujumu uchumi dhidi ya raia hao wawili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es salaam kwa mashitaka matatu ya kula njama ya kutenda kosa, kuendesha upatu na utakatishaji fedha.

Kwa kuwa watuhumiwa walikuwa hawajakamtwa, upande wa Jamhuri uliomba hati ya kuwakamata.

# Ajinyonga na kufa baada ya kumpoteza mtoto

**Na Manuel kaminyoge,** SONGWE

WANANCHI wa kijiji cha Ihanda, Mbozi mkoani Songwe, wamekumbwa na taharuki baada ya kumkuta Ezekiel Mela, anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 30 akiwa amejinyonga hadi kufariki dunia.

Mela amejinyonga zikiwa zimepita siku chache baada ya kifo cha mtoto wake kinachosemekana kilikuwa katika mazingira ya utata hivyo kumfanya kuwa na mawazo mengi.

Aikael Kibona, mke wa marehemu, akisimulia kwa masikitiko, alisema tukio hilo lilimshitua kwa kuwa hawajawahi kutofautiana wakati wote wa maisha vyao na juzi akitoka kazini alikuwa sawa na hakuonyesha shida yoyote .

Mkewe huyo alisema jana asubuhi kulipokucha, waliagana vizuri na akienda kazini na yeye akabaki nyumbani lakini baada ya muda mfupi alipigiwa simu kuwa mume wake amefariki dunia kwa kujinyonga na kamba. "Mume wangu hatujawahi kukosana hata mara moja na leo (jana) ameniaga vizuri na mimemtakia kazi njema kumbe ndiyo anakwenda kujiua! Imeniuma sana mimi. Nimempoteza mtoto majuzi tu tena leo mume! Mungu nisaidie," alisema.

Ezekiel Sichone, mmoja wa wananchi waliofika eneo la tukio, alisema tukio hilo limewashtua sana na kuibua taharuki miongoni mwao.

Sichone aliongeza Mela hakuwa mtu wa kushilikisha changamoto alizokuwa nazo japo alikuwa akilalamika sana tukio la mtoto wake kupoteza maisha kwa mazingira ya kutatanisha.

"Huyu jamaa ni ngumu kujua chanzo cha kifo chake kwani alikuwa mtu ambaye hakuwa tayari kumweleza mtu changamoto aliyonayo licha ya kuwa alikuwa akiongelea sana tukio la kifo cha mtoto wake ambacho nacho kilikuwa cha kutatanisha," alisema Sichone.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ihanda, Nico Mwaiswelo, alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa moja asubuhi ambapo alifika eneo la tukio na kukuta umati wa watu .

Alisema matukio kama hayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara yakiwamo ya watu kujinyonga, kunywa sumu na mauaji huku akiwataka wananchi kuacha kuchukua uamuzi mgumu .

Diwani wa Viti Maalum Tarafa ya Vwawa, Crescensia Kapange, aliwataka vijana kutochukua uamuzi mgumu huku akiongeza kuwa katika kijiji hicho kumekuwa na matukio mengi ambayo yanatoa taswira mbaya.




Katibu wa kikundi cha wafanyabiashara soko kuu la Manispaa ya Iringa, Aldo Kaduma (kushoto), akimkabidhi mfanyabiashara wa soko hilo, Batsta Ngede, msaada wa ndoo za maji na vifaa mbalimbali kwa ajili ya kujikinga na virusi vya corona vilivyotolewa na mmiliki wa Nana's Café, jana **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mbunge ataka vyombo vya dola viwalinde waliowekwa karantini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wameitaka serikali kuhakikisha Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola vinaimarisha ulinzi kwenye maeneo yanayotumika kuwaweka chini ya uangalizi watu wanaotoka katika nchi zilizoathiriwa na ugonjwa wa corona.

Vilevile, serikali imesema barakoa za kitambaa hazizuii na hazimkingi mtu kupata virusi vya corona huku baadhi ya wabunge wakishauri matumizi ya dawa za miti shamba zinazodaiwa kutibu ugonjwa huo.

Akichangia bungeni jijini hapa jana hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka ujao wa fedha, Mbunge wa Mchinga (CUF), Hamidu Bobali, alisema ulinzi unapaswa kuimarishwa kwenye hoteli ambazo watu wanawekwa karantini kutokana na kuwapo kwa taarifa kwamba hawakai siku zote zinazotakiwa.

"Tusiachie walinzi wa hoteli, ziko taarifa kuwa wamekuwa hawakai siku zote na wamekuwa wakiondoka, kuna haja ya kuchukua hatua zaidi kama taarifa hizi ni za kweli.

"Nchi za Uganda na Kenya zimechukua hatua za kuwaachia majeshi kulinda hoteli hizi kwa sababu jambo hili ni la kiusalama," alisisitiza.

Katika mjadala huo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alilazimika kusimama na kutoa ufafanuzi kuhusu matumizi ya barakoa, akibainisha kuwa za kitambaa hazizuii wala hazimkingi mtu kupata virusi vya corona.

"Tuwe waangalifu kwa matumizi ya barakoa, zitumike zilizoshauriwa na wataalamu, huu ugonjwa hausambazwi kwa hewa bali kwa maji maji yakiwamo yanayotokana na chafya, hizo barakoa za kitambaa hazizuii na hazimkingi mtu kupata virusi vya corona," alisema.

Dk. Ndungulile alitoa ufafanuzi huo kutokana na mchango wa Mbunge wa Sumve (CCM), Richard Ndassa, ambaye alisema serikali iliangalie kwa makini suala la corona na kwamba kirusi cha corona ni tofauti na vingine, hakishikiki hivyo bei ya barakoa haipaswi kuwa kubwa.

"Kuna barakoa za kitambaa kwa ajili ya wanafunzi wa shule ambazo bei yake ni Sh. 500 na inazuia," alisema.

**TIBA KIENYEJI**

Mbunge wa Sengerema (CCM), William Ngeleja, alisema kumekuwapo na taarifa kuwa kuna tiba ya kienyeji ya mafua ya kujifukiza.

"Sijaelewa kitu gani kimetukumba kama taifa, pale Muhimbili kuna kitengo cha tiba mbadala, yaliyofanyika China hadi kudhibiti ugonjwa huu ni siri, si yote yanajitokeza lakini ninachotaka kusisitiza wewe Spika unaweza kutumia Kanuni ya Tano kutoa mwongozo kwa serikali na ikatafakari. "Kwanini tiba mbadala ya kimapokeo ambayo wengi tumetibiwa na kupona kwa miaka mingi hatuipi nafasi katika vita hii? Tuna corona hapa ambayo ni janga la kidunia, hili janga kila nchi ipambane kwa mazingira yake.

"Hili jambo serikali inaweza 'kuli-promote' Watanzania wakafanya, kila mtu akajifukize asubuhi na familia yake, kuna hasara gani tukajifukizia na tukapata nafuu, lakini itatokea nini kama kujifukiza kunatibu, lakini hatuipi nafasi hii? Naomba Spika litafakariwe vizuri," alisema.

Kutokana na kauli hiyo, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema: "Hii kujifukizia hata ugogoni ipo, siyo ya Kanda ya Ziwa peke yake na haihitaji kujifukizia kila siku, unaweza fanya kwa wiki mara moja au mara mbili, sasa wabunge mmepata 'tipu' ya bure hiyo, lakini msijifukizie yasiyofukiziwa."

Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Hawa Mwaifunga, aliomba kuangaliwa matangazo yaliyopo kwenye mitandao ya kijamii kuhusu matumizi ya miti shamba.

"Unakuta mtu anakwambia chemsha hiki chemsha hiki, jamani tutauana, mwingine anachukua ndimu anaweka katika glasi mtu akisikia inasaidia anafanya, serikali mtusaidie janga hili ni baya sana," alisema.

Mbunge wa Muleba, Prof. Anna Tibaijuka, alisema jamii inahitaji kuishi kwa tiba mbadala.

"Hakuna mtu atakayesubiri afe, makabila mbalimbali yana mbinu za kukabiliana na homa za mapafu, corona ni virusi vipya, lakini siyo mara ya kwanza kwa virusi kama hivyo kutokea na hivyo kufukizia ni muhimu," alisema.

Alisema ili kujifukiza, unahitaji mkaa, kuni na ili kupata tiba hizo za asilia, ni lazima uwe karibu na joto.

"Nimemwandikia barua rasmi Naibu Waziri Ndungulile ili waangalie chaguo B mbali na kuangalia pia chaguo A kwa kuvaa mask na nyingine.

"Mfano wa nchi ya Ghana, tayari watu 33 wamepona wametumia mwarobaini, madaktari wengi wana elimu ya Ulaya na wamekuwa wakibeza tiba asilia.

"Serikali tuangalie plan A na B, na kama tukizidiwa, Wapogoro tunafanyaje? Wagogo tufanyeje?" Profesa Tibaijuka alihoji.

# Watoto wazagaa kila kona bila kujali hatari ya corona

## ■ Wengi wazurura mitaani, baadhi wawa ombaomba na kusaidia wazazi kazi na biashara

**Waandishi Wetu**

LICHA ya serikali kufunga shule kutokana na tishio la corona, watoto wengi wameonekana kuzurura, kutumikishwa sokoni na maeneo mengi huku wazazi wakishindwa kuwadhibiti watoto wao.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe katika mikoa mbalimbali umeonyesha kuwa baadhi ya maeneo wazazi bila woga, wanawatumikisha kwa kuwapa biashara watoto wao ambazo wanaziuza maeneo yenye mikusanyiko.

Katika maeneo mengine, watoto wameonekana mitaani wakiendelea na michezo yao mbalimbali ikiwamo mpira wa miguu, licha ya kwamba serikali imekuwa ikisisitiza masuala ya mikusanyiko yasiwepo.

Aidha, watoto wameonekana kwenye masoko wakifanya biashara mbalimbali ambazo wameelekezwa na wazazi au walezi wao.

Katika mkoa wa Mwanza, baadhi ya wazazi wameonekana kuwatumia watoto wao kwa kuwapa biashara ndogo na kwenda kuziuza kwenye maeneo yenye mikusanyiko.

Mkuu wa Mkoa huo, John Mongella, alisema licha ya serikali kuzifunga shule, baadhi ya wazazi wameshindwa kuwadhibiti watoto wao na kuwaachia wakirandaranda mtaani.

"Wazazi mtambue watoto hawajafunga shule bali wamerudishwa nyumbani kwa sababu ya corona. Wasitumie nafasi hiyo kuwafanyisha kazi zinazosababisha kuzurura mitaani," alisema.

Aidha, alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama, wakiwamo mgambo, watumie muda wao kutoa elimu kwa wananchi.

Mratibu wa Shirika la Msalaba Mwekundu mkoani humo, Salome Tuppa, alisema lengo lao ni kuwapatia elimu wananchi ili wawe na utayari.

Naye Meneja wa Wakala ya Huduma za Ufundi na Umeme Tanzania (Temesa), mkoani humo, Mhadisi Karonda Hassan, aliiomba serikali iwapatie vipimo vya kupimia dalili za ugonjwa huo katika kivuko cha Kigongo na Busisi.

Mkurugenzi wa Shirika la Kivulini, Yassini Ally, na Rehema Sabiri mkazi wa Butimba, walitaka wazazi waelimishwe kuhusu kutoambatana wa watoto wao sehemu zenye mikusanyiko.

Uchunguzi uliofanywa kwenye maeneo ya Chang'ombe, Chidachi jijini Dodoma, umeonyesha watoto wakiwa kwenye makundi wakicheza michezo yao ya kila siku.

Fatuma Ally, mmoja wa wazazi mkoani humo, aliliambia gazeti hili kuwa, wazazi inawawia vigumu kuwafungia ndani watoto kwa sababu wamekuwa wakifanya uharibifu wa vitu.

Alisema hilo litawezekana baadhi ya maeneo ambayo nyumba zake zina uzio lakini kwenye eneo lenye idadi kubwa ya watu ni vigumu.

**DIWANI ATAKA ELIMU**

Naye Diwani wa Mailimoja, Mkoa wa Pwani, Ramadhani Lutambi, alisema bado kunahitajika elimu kwa watoto kuhusu vizuri vya corona.

"Serikali imezifunga shule ili watoto wawe kwenye uangalizi wa wazazi nyumbani lakini ni vyema elimu iendelee kutolewa kwa wazazi ili kuwadhibiti watoto wao," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mailimoja B, Shauri Yombayomba, alisema wanatarajia kufanya kikao na wazazi ili kuwapa maelekezo namna ya kujilinda wao na watoto wao dhidi ya corona.

"Wakati watoto wakionekana mtaani wakizurura, wazazi nao wanakwenda sehemu za starehe bila ya hofu, kikubwa ni elimu ambayo tunatarajia kuitoa," alisema.

**DAR SHIDA**

Mkazi wa Mtaa wa Kilungule, Bunju jijini Dar es Salaam, Lucy Mnzava, alisema katika mtaa huo bado hakuna udhibiti mzuri wa watoto kutulia nyumbani.

"Bado kuna watoto wengi ambao wanaonekana wakizurura mtaani wengine tunawaona wakicheza mpira na tatizo wazazi bado hawajawaambia na ukiwaambia kuwa waende nyumbani kuna ugonjwa wa corona hawaelewi," alisema.

Katika maeneo ya Kimara, Nipashe ilishuhudia watoto wakiendelea kucheza mtaani na baadhi yao walipoulizwa walikiri wazazi wao kuwaeleza kuwa kuna ugonjwa wa corona.

Aisha Mwasha, mmoja wa wazazi maeneo hayo, ambaye alisema elimu dhidi ya corona na namna inavyoambukiza ameitoa kwa watoto wake, lakini changamoto ni kwamba hawazuiliki.

Mkazi wa Tabata, Bahati Saidi, alisema ili kuzuia watoto kukaa kwenye mikusanyiko wameamua kuwapeleka elimu ya ziada (tuition)

"Akienda na kurudi huwa ananawa na kitakasa mikono na huwa ninamuelimisha kila mara ya namna ya kujilinda na corona," alisema.

Naye mwalimu aliyejitambulisha kwa jina moja la Isack, mkazi wa Tabata Kimanga, alipoulizwa kuhusu mafunzo ya ziada kwa watoto huku kukiwa na katazo la mikusanyiko, alisema anachofanya ni kuwasaidia kielimu.

"Kama mnavyojua watoto pindi wawapo likizo huwa hawana utaratibu wa kujisomea na wanapofungua shule husahau vitu vingi waliyofundishwa," alisema.

Alisema ili kuwakinga na corona wameweka utaratibu wa kunawa mikono kabla na baada ya masomo.

Mwanaisha Ally, mkazi wa Mwenge, alisema katika mtaa wao watoto wamedhibitiwa na wazazi na kama ni kucheza kila mmoja anacheza nyumbani kwake.

"Sijaona watoto wakiwa kwenye makundi, labda mmoja mmoja ambao wanatoka kwa kutumwa na mzazi dukani, wazazi wameweza kuwadhibiti," alisema.

Katika maeneo ya Sinza, gazeti hili lilishuhudia mtoto mmoja mmoja mtaani huku John Stanslaus, mkazi wa eneo hilo, alisema hatari ya corona imewafanya wazazi wengi kuwafungia kwenye mageti watoto wao..

**DC AWEKA MTEGO**

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema wameagiza walimu shule zikifunguliwa watoto wapewe mtihani wa majaribio ili kuwapima kama walipokuwa nyumbani walikuwa wakijisomea au kuzurura mtaani.

"Tumetoa maelekezo kwa maofisa elimu kata na watendaji wa wata, kuhakikisha wanafunzi hawazururi mitaani. Elimu hii pia tunaitoa kwenye nyumba za ibada," alisema.

Mzazi Jackson Mapolu, alisema kuzuia mtoto kuzurura ni vigumu kwa sababu wazazi walio wengi wakati wa mchana huwa kwenye shughuli za kujitafutia kipato.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Mkoani Iringa, Mkuu wa wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, alisema suala la virusi vya corona ni kubwa na wazazi wasichukulie poa juu ya tahadhari mbalimbali zinazotolewa na serikali. Alisema lengo la serikali kutangaza kuzifunga shule zote na vyuo ni kutaka watoto hao kutulia nyumbani kuepuka misongamano inayoweza kusababisha kupata maambukizi ya corona.

Hivyo aliagiza wazazi wote wenye watoto kuwazuia nyumbani na kuwakanya kuzurura ovyo mitaani au kwenda kwenye mikusanyiko kwa kuwa ni rahisi kupitia mikusanyiko hiyo kupata maambukizi

Kasesela alisema wakati huu wa likizo kwa ajili ya hofu ya corona ni vizuri watoto hao kila mmoja kutulia nyumbani badala ya wazazi kuwaacha wakiendelea kuzunguka mitaani ambako si salama.

Pia alisema serikali kupitia idara zake za afya imechukua tahadhari mbalimbali za kuwalinda wananchi dhidi ya virusi vya corona kwa kutoa elimu pamoja na kuanza kupuliza dawa katika maeneo yote yenye mikusanyiko kama stendi.

Frank Ndelwa, mkazi wa Miyomboni, alisema watoto wanaonekana mtaani wakifanya kazi ya ombaomba kwa kisingizio cha maisha magumu nyumbani kwao.

Ndelwa aliiomba halmashauri kuwatumia mgambo kuzunguka mitaani kuwakamata watoto wote wanaoonekana mitaani na kuwachukulia hatua kali wazazi wao ili kuwaepusha corona.

Naye Naibu meya wa Halmshauri ya Manispaa ya Iringa, Joseph Ryata, alisema kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa imeendelea kutoka elimu mbali mbali juu ya tahadhari ya virusi vya corona na tayari wamekwisha wakutanisha maofisa watendaji wote wa kata na mitaa ili waende kutoa elimu kwa wananchi wanaowaongoza .

**Imeandaliwa na Renatha Msungu, (Dodoma), Julieth Mkireri, (Kibaha), Neema Emmanuel, (Mwanza), Marco Maduhu (Shinyanga), Francis Godwin (Iringa),Mary Geofrey, Elizabeth Zaya na Romana Mallya (Dar).**

# Serikali yasema hakuna upigaji NIC

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema hakuna ubadhirifu wowote unaoendelea katika Shirika la Bima la Taifa (NIC) na shirika limeendelea kuboresha mifumo yake ya udhibiti wa mapato na matumizi,ili kukabiliana na washindani wake kibiashara katika sekta ya bima.

Hayo yalibainishwa na jana bungeni jijini hapa na Wizara ya Fedha na Mipango ilipojibu swali la Mbunge wa Ubungo, Saed Kubenea (Chadema), aliyetaka kujua ukweli wa taarifa kwamba ubadhirifu bado unaendelea katika shirika hilo na halina mipango thabiti ya kukabiliana na washindani wake kibiashara.

Katika majibu yake, wizara hiyo ilisema kuwa, katika kujiimarisha kibiashara, shirika limechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kwa kutumia Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (GePG), ulioanza kutumiwa na shirika Novemba mwaka jana na kuondoa ukusanyaji wa mapato kwa fedha taslimu. Ilisema hatua nyingine zinazochukuliwa ni kuongeza udhibiti katika ulipaji wa madai na kufanya ukaguzi maalum wa madai yote ya Bima za Maisha ili kujiridhisha juu ya uhalali wa madai hayo.


"Shirika lipo katika hatua za mwisho za kuunganishwa na Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kihasibu na Malipo katika Taasisi za Umma (Muse) ambao utaongeza udhibiti katika malipo yote yanayofanyika, kusitisha matumizi ya hundi ambapo kuanzia Desemba 2019, shirika lilisitisha matumizi ya hundi katika malipo yake yote na kuanza kutumia mfumo wa malipo wa kielektroniki, hivyo kuongeza uthibiti wa matumizi na kuzuia uwezekano wa matumizi ya hundi feki," ilisema.

Wizara hiyo iliongeza kuwa serikali pia imechukua hatua mbalimbali kuliimarisha shirika hilo kitaalamu kwa kuliondoa kwenye mashirika yaliyotakiwa kubinafsishwa na kuliwezesha kushiriki katika biashara ya bima kwa ushindani pamoja na kulifanyia mabadiliko ya kiuongozi ili kuongeza tija na kuleta mabadiliko chanya kwenye utendaji na usimamizi wa shughuli zake.

Ilisema hatua zingine zilizochukuliwa ni kulisaidia shirika kwa kulipatia wataalamu mbalimbali katika nyanja za mifumo ya Tehama, utendaji kazi na utunzaji kumbukumbu (e-office) ili kuongeza ufanisi wa shirika na kukabiliana na ushindani wa kibiashara.

"Serikali pia imeliimarisha shirika kifedha kwa kuchukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kupata biashara za serikali na kushinikiza malipo ya hapo kwa hapo ya premium ambayo yamesaidia kupunguza malimbikizo ya premium kutoka kwa taasisi za serikali kutoka zaidi ya Sh. bilioni 20 hadi milioni 500 kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020," wizara hiyo ilibainisha.

Ilisema pamoja na maendeleo mazuri ya shirika, serikali inaendelea kuliimarisha shirika hilo la kimkakati kwa kulisaidia katika kupitia upya mpango mkakati wake ili uendane na mahitaji halisi ya biashara ya ushindani, kuongeza uwekezaji katika mifumo ya Tehama kwa lengo la kuwafikia wateja wengi zaidi, kuongeza ubora wa huduma zake na kulipa madai haraka na kwa urahisi, kujitangaza zaidi na kuongeza uwekezaji wenye tija ili kutoa gawio kubwa kwa serikali na kushiriki katika shughuli za maendeleo ya taifa.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisalimiana na Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Utetezi wafunga ushahidi kesi ya Zitto

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uchochezi inayomkabili Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, umefunga ushahidi baada ya kuita mashahidi wanane akiwamo mshtakiwa huyo.

Wakili wa utetezi, Jebra Kambole, alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaid, kuwa utetezi umefunga ushahidi na kwamba hawana shahidi mwingine.

Kambole aliiomba mahakama nakala ya mwenendo wa kesi kabla ya kuwasilisha hoja za majumuisho ya mwisho ya kama Zitto ana hatia au la.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri, ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, ulipinga hoja hiyo kwamba hawaoni sababu ya kusubiri mahakama itoe mwenendo wa kesi kwa kuwa pande zote mbili zilikuwa zikiweka kumbukumbu wakati wanasikiliza ushahidi huo.

Kweka alidai kuwa kusubiri mwenendo wa kesi ni kupoteza muda.

"Mheshimiwa tunapinga hoja ya utetezi kwa sababu ni kuchelewesha haki, kwani wote tulikuwa tukiweka kumbukumbu ya mwenendo wa kesi hii. Kwa hiyo Jamhuri tunaomba tuendelee na hatua ya kuwasilisha hoja za majumuisho," alidai Kweka.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Hakimu Shaidi alisema kuwa kusubiri kutolewa kwa mwenendo huo kutachelewesha hukumu kwa kuwa taratibu za kuchapa mwenendo huo zitachukua muda mrefu.

Alisema pande zote mbili ziwasilishe hoja za majumuisho ya mwisho Aprili 28, mwaka huu, na kesi hiyo itatajwa tena Aprili 29, kwa ajili ya kupangwa tarehe ya hukumu.

Mapema mahakamani hapo, upande utetezi uliita mashahidi wanane na Jamhuri 15.

Katika kesi ya msingi, Zitto anadaiwa Oktoba 28, 2018 akiwa katika mkutano na waandishi wa habari, uliyofanyika katika Makao Mkuu ya ofisi ya Chama cha ACT Wazalendo, alitoa maneno ya uchochezi yenye kuleta hisia ya hofu na chuki.

Ilidaiwa kuwa mshitakiwa alitamka kuwa: "...watu ambao walikuwa ni majeruhi katika tukio la mapambano baina ya wananchi na Polisi wakiwa wamekwenda hospitali kupata matibabu katika kituo cha afya Nguruka, Polisi wakapata taarifa kuwa kuna watu wanne wamekwenda hospitali kituo cha afya Nguruka kupata matibabu wakawafuata kule wakawaua."

Katika shitaka ya pili ilidaiwa Oktoba 28, mwaka huu maeneo ya Kijitonyama katika makao makuu ya chama hicho, jijini Dar es Salaam, alitoa maneno ya uchochezi dhidi ya Jeshi la Polisi akisema: "... lakini tumefuatilia kwa kina jambo hili, taarifa ambazo tumezipata kutoka kijijini Mpeta-Nguruka, Uvinza ni mbaya.

Ni taarifa ambazo zinaonyesha wananchi wengi sana wameuawa na jeshi la Polisi pamoja na kwamba afande (Simon) Sirro amekwenda kule, haijatoa taarifa yoyote kuhusu wananchi...kama hawa wanyantuzu walivamia eneo la Ranchi kuna taratibu za kisheria za kuchukua na sio kuwauwa, wananchi wengi sana wamekufa."

Ilidaiwa kuwa katika tarehe hiyo hiyo, Zitto alitoa maneno ya uchochezi dhidi ya Jeshi la Polisi akisema: "... Tumekuwa tukifuatilia kwa kila yanayojiri yote huko Uvinza tunasikitika kusema kuwa taarifa tunazozipata kutoka Uvinza zinaogofya mno kwani tunaambiwa kuwa wananchi zaidi ya 100 wa kabila la Wanyantuzu wamepoteza maisha kwa kupigwa risasi na Polisi, wengine wakisema kuuawa hata wakiwa kwenye matibabu hospitalini baada ya kujeruhiwa kwenye purukushani na jeshi la polisi."

**"...watu ambao walikuwa ni majeruhi katika tukio la mapambano baina ya wananchi na Polisi wakiwa wamekwenda hospitali kupata matibabu katika kituo cha afya Nguruka, Polisi wakapata taarifa kuwa kuna watu wanne wamekwenda hospitali kituo cha afya Nguruka kupata matibabu wakawafuata kule wakawaua."**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi ya fainali za CHAN yasisimamishwe

**TIMU** ya soka ya Taifa (Taifa Stars), imefanikiwa kukata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Taifa Stars inafanikiwa kupata tiketi ya kushiriki fainali hizo kwa mara ya pili, mara ya kwanza ilikuwa ni mwaka 2008, wakati kikosi hicho kikiwa chini ya Kocha Mkuu Mbrazili Marcio Maximo.

Awali fainali hizo zilitarajiwa kufanyika kuanzia Aprili 4 hadi 25, mwaka huu katika miji mitatu ya Cameroon ambayo ni pamoja na Yaounde, Douala na Limbe, lakini zimesogezwa mbele kufuatia kuwapo kwa maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Tayari droo kwa ajili ya kupanga ratiba ya fainali hizo ilishafanyika na kila nchi inafahamu wapinzani wake.

Taifa Stars ilipata tiketi ya kushiriki fainali hizo baada ya kuwaondoa majirani zetu Kenya (Harambee Stars) na Sudan ambayo pia iko kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Taifa Stars inatakiwa ijiandae vizuri ili ikafanye vema katika fainali hizo, tofauti na ilivyokwenda kwa mara ya kwanza.

Ili Stars ikapeperushe vizuri bendera ya nchi, inatakiwa kuandaa maandalizi ya muda mrefu na kamwe tusisubiri siku chache na kufanya mazoezi ya zimamoto.

Nipashe imeamua kukumbusha kuhusu maandalizi ya timu hiyo, kwa sababu inaamini maandalizi bora ndiyo yanayotoa matokeo chanya na tusiige maandalizi kama yanayofanywa na timu za mataifa mengine.

Nchi nyingine timu zao zinaundwa na wachezaji wengi wanaojielewa na kujitunza na wanafahamu umuhimu wa kufanya vizuri.

Katika mafanikio hakuna njia ya mkato, ni lazima Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kushirikiana na Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije kuandaa programu mbalimbali za muda mrefu na mfupi mpaka hapo tarehe mpya itakapotangazwa.

Wachezaji wa Stars wapewe maandalizi yanayolingana na ukubwa wa michuano hiyo ambayo binafsi pia itasaidia kutangaza vipaji vyao.

Kama ambavyo makocha wa timu za Ligi Kuu Bara au Ligi Daraja la Kwanza wanavyoendelea kuwanoa wachezaji wao kupitia njia nyingine na si ya mazoezi ya pamoja, Ndayiragije pia anatakiwa kuwezeshwa ili kutekeleza majukumu yake na hatimaye michuano ikifika, vijana wake wanakuwa wako tayari kupambana.


Inajulikana idadi kubwa ya wachezaji watakaounda kikosi hicho watatoka kwenye Ligi KuuBara, hivyo uamuzi wowote utakaofanywa baada ya kurejea ligi, uzingatie maendeleo na viwango vya nyota hao wanaotarajiwa kuitwa na Ndayiragije.

Ni muda sahihi kwa TFF kukaa karibu na vilabu vyake na kuwaeleza umuhimu wa kufuatilia kwa karibu viwango vya wachezaji kwa faida na maslahi ya taifa ambalo sasa linataka kwenda CHAN kushindana na si kusindikiza.

Wachezaji wenyewe pia wakumbuke fainali hizo ni sehemu nyingine muhimu ya wao kujiweka 'sokoni' kwa sababu huvutia mawakala mbalimbali kutoka Ulaya.

Wachezaji nyota wanaong'ara sasa Ulaya kutoka nchi za Afrika Magharibi wamepata timu kupitia fainali za CHAN au AFCON, hivyo Watanzania pia tutumie fursa hii kwa sababu hakuna kisichowezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kipendacho moyo ni dawa

Na Barnabas Maro

**KITU** anachokipenda mtu au inachokipenda roho ya mtu huwa kama dawa yake.

Methali hii yaweza kutumiwa kumpigia mfano mtu anayeelekea kukipenda kitu fulani sana ingawa wengine wanakiona kibaya.

Wengine husema "Kipenda roho hula nyama mbichi." Maana yake roho ikipenda huweza kula hata nyama mbichi. Matumizi yake ni sawa na "Kipendacho moyo ni dawa."

S.A. Mohamed ameandika hivi kwenye kitabu chake cha Vito vya hekima, Simo na Maneno ya Mshangao: "Pavumapo palilie si kazi kudamirika*.

*Damirika ni kitendo cha kitu au maisha ya mtu kuharibika kabisa; fisidika. 'Damiri' ni angamizwa kabisa; haribikiwa.

Duniani kuna vyakula vya aina nyingi lakini si vyote vinavyopendwa na watu wote. Kwa mfano kuna wasiokula nyama ya kondoo, bata, mbuzi wala utumbo. Mwandishi wa makala haya ni miongoni mwao.

'Mchezo' ni jambo ambalo watu au timu hulifanya kwa kushindana ili kupata mshindi. Kwa mfano, mpira wa miguu uliopewa majina mengi: kandanda, kabumbu, soka, dimba n.k., watu huhitilafiana kila mmoja akiwa na sababu zake.

Mfano mzuri ni wale wanaojipaka rangi za bendera za timu zao, kujiandika kwenye miili yao na wengine kuvaa vitu vya ajabu ajabu kuonyesha jinsi wanavyozishabikia timu zao.

Mbali na hayo, kuna wanaopigana uwanjani, wanaong'oa viti wanavyokalia, wanaolia na kutoa machozi, wanaozirai na waliopoteza maisha!

Kadhia (jambo linalojiri; tukio la kuhuzunisha) hii hutokea wakati timu zao zinapofungwa, hasa na wapinzani wao. Hii hutokea mara kwa mara zipambanapo Yanga na Simba.

Hata hivyo yanipa shida kubainisha (kitendo cha kutofautisha miongoni mwa vitu au watu) kama hali hiyo husababishwa na mshituko wa moyo timu zao zinapofungwa au ni kutokana na kupoteza dau (fedha au kitu anachoahidi mtu kutoa kwa timu itakayoshinda).

Ndo maana wahenga walisema: "Tamu ikizidi tamu huwa si tamu tena." Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba jambo lolote zuri huwa na mipaka. Linapozidi huwa halivutii tena.

Sasa ni kwa nini baadhi ya watu hupenda sana timu fulani? Mara nyingi, katika mchezo wowote watu humpenda mchezaji anayefanya vizuri kwenye mashindano.

Mchezo wa ngumi, kwa mfano, watu walimpenda mno Mohamed Alli (Mungu amrehemu) wa Marekani aliyekuwa bingwa wa mchezo huo duniani. Hata waliokuwa hawaupendi mchezo huo walijikuta wakiupenda kwa sababu ya Mohamed Alli.

Baada yake alifuatia bondia Mike Tyson pia wa Marekani aliyetikisa ulimwengu wa masumbwi kama alivyokuwa marehemu Mohamed Ali. Kadhalika alipendwa na wengi duniani.

Nchini Tanzania kuna waliopendwa na wengi ila sasa anayezungumzwa na kupendwa na wengi si mwingine ila ni mgosi Hassan Mwakinyo wa Tanga anayeitangaza nchi kwa mchezo huo wa ngumi.

Sababu ya wachezaji au timu kupendwa hutokana na juhudi na ushindi hivyo hupendwa na wengi ingawa katika hao wapo wanaofuata mkondo tu. Mchezaji akishuka au timu ikipoteza mwelekeo, baadhi ya watu huhamia kwingine!

Timu ya Manchester United ya Uingereza ilitikisa ulimwengu wa soka hata mwalimu wao, Alex Ferguson akatunukiwa jina la 'Sir' na Malkia Elizabeth wa nchi hiyo.

Humu nchini timu zenye mashabiki (watu wenye mapenzi na hamasa kubwa) wengi ni Yanga na Simba. Wingi wa mashabiki wao ni tofauti na wanachama wenye kadi na waozichangia timu hizo, mbali ya wale wanaozisaidia kwa hali na mali.

Mashabiki wengi wa timu hizi wanapoona hazifanyi vizuri, huzikimbia kwani wanachotaka ni ushindi tu! Hawajui kuwa kuna sare (kufungana idadi sawa), suluhu (kutofungana) kushinda na kushindwa?

Wahenga walirahisisha zaidi waliposema: "Hakuna mume wa waume." Maana yake hakuna mtu mmoja anayeweza kuwashinda wanaume wenzake wote. Methali hii hutumiwa kwa mtu anayejitia ubabe au anayejidai kuwa na nguvu kama njia ya kumnyamazisha.

Yanga ndio waliozitesa timu zingine, kwa kuwa mabingwa mara nyingi mpaka kuitwa 'mabingwa wa kihistoria.' Upepo umebadilika na sasa timu inayotamba nchini ni Simba, wanaoitwa 'mnyama wa Msimbazi' kwa mwaka wa tatu mfululizo wakati Yanga wakisota kwa kipindi kama hicho bila kuwa bingwa!

"Kupata kuna Mungu." Mtu anayetaka kufanya jambo hushajiishwa na msemo huu. Haifai mtu kusitasita katika kuomba jambo au kupigania jambo.

Ni bora mtu kuondoa wasiwasi. Woga na ujasiri wa kuona labda hatofuzu. Tukijaribu matendo ya ujasiri, mbele yetu tumweke Mungu. Yeye ndiye atoaye na ndiye anyimaye.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Mgonjwa mwingine apona corona

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amethibitisha kupona kwa mgonjwa wa tatu aliyekuwa na maambukizi ya ugonjwa wa corona nchini na kuruhusiwa kurudi nyumbani, huku mgonjwa mwingine mmoja akisubiri uthibitisho wa kipimo cha tatu.

Ummy aliyasema hayo jana katika taarifa yake kwa vyombo vya habari kuhusu maendeleo ya ugonjwa huo nchini na kusema kuwa mgonjwa anayesubiri kipimo cha tatu, kipimo cha pili kimeonyesha hana tena virusi vya corona.

Alisema mgojwa aliyepona ni mwanamume mwenye historia ya kutembelea kikazi Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC) na Burundi na alikuwa katika moja ya kituo cha matibabu wilayani Ngara mkoani Kagera na kwamba mkoa huo hauna tena mgonjwa.

"Arusha tulikuwa na wagonjwa wawili, mmoja aliruhusiwa na mgonjwa mwingine majibu ya leo asubuhi (jana) yameonyesha kuwa ni 'negative' (hana maambukizi) hivyo tunasubiri kipimo kingine kimoja ili aweze kuruhusiwa," alisema Ummy.

Kadhalika Waziri Ummy, aliwashukuru wananchi kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa Corona hususani kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka.

Aliwataka wananchi kuendelea kuepuka mikusanyiko na misongamano isiyo ya lazima ili kukabiliana na maambukizi.

"Nawaomba kukaa mita moja au zaidi kati ya mtu mmoja na mtu mmoja ili kuzuia maambukizi zaidi," alisisitiza Ummy.

Katika hatua nyingine, Ummy amekabidhi vifaa kinga kwa Jeshi la Polisi na Magereza kwa ajili ya kujikinga wakati wa kutoa huduma kwa jamii ikiwa ni msaada kutoka Taasisi ya Jack Maa ya China.

Alisema licha ya asilimia 90 ya vifaa kinga kuelekezwa kwa watumishi wa afya katika vituo vya huduma ya afya nchini, kipaumbele cha Serikali ni kuwakinga watumishi wa afya.

"Juzi tulimsikia Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) na mimi nataka kutumia fursa hii kueleza kwamba sisi Serikali tutaendelea kuwalinda watumishi wa afya ili wasipate maambukizi wakati wanapotoa huduma kwa wagonjwa," alisema Ummy.

Alivitaja vifaa kinga hivyo ni barakoa 16,000 kwa Jeshi la Polisi na Magereza, gloves 8,000, nguo za kijikinga (PPE) 50 na jiki ya vidonge kopo (chlorine) 100.

Alisema kuwa wizara yake imetoa vifaa hivyo kwa sababu Jeshi la Polisi na Magereza wamekuwa wakikutana mara kwa mara na wananchi na pia wamekuwa wakisaidia kazi mbalimbali za kuhudumia jamii ikiwamo kutoa huduma za afya kwenye vituo vyao.

Waziri Ummy Mwalimu alisema kuwa vifaa hivyo vitatumika kwa ajili ya vituo vya afya vya Jeshi na kwa ajili yao wenyewe wakati wa kutoa huduma kwa wananchi.

"Lengo letu ni kuhakikisha pia kwamba vituo vyote vinatoa huduma kwa jamii hususani Jeshi la Polisi na Magereza tunawapatia vifaa tiba ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona," alisema Ummy.


Baada ya kukabidhiwa vifaa kinga kutoka kwa Waziri wa Afya, Naibu Kamishina wa Jeshi la Polisi na Mkuu wa Utawala wa Jeshi hilo, Anthon Ruta, alishukuru kwa kubabidhiwa vifaa kinga kwa ajili ya kuendeleza mapambano dhidi ya ugonjwa vya Corona na kuvitumia kutokana na maelekezo yenu.

Naye Mkaguzi Msaidizi na Ofisa Tabibu wa Jeshi la Magereza, Kenazi William, alishukuru kwa kupatiwa msaada kwa kuwa wamekuwa wakipokea wageni wengi wakiwamo mahabusi, wafungwa na kuchangayikana na pia vifaa hivyo vinawapa nguvu zaidi katika kukabiliana na ugonjwa corona.

Hadi jana hakukuwa na taarifa ya mgonjwa mpya aliyetangazwa na Serikali hivyo kufanya taarifa ya wagonjwa waliobainika nchini kuwa ni 20.

Kati ya wagonjwa hao 20, mmoja alifariki dunia wiki hii na watatu wameshadhibitishwa kupona na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa wanaoendelea na matibabu kuwa ni 16.

Kadhalika kwa mujibu wa wizara ya afya, jumla ya watu 561 wanafuatiliwa , watu 184 wameshakaa chini ya uangalizi wa siku 14 lakini hawajakutwa na maambukizi wakati wengine 130 wakiwa chini ya uangalizi wa lazima (karantini).



Mafundi ujenzi wakiondoa udongo ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuweka zege kwenye barabara korofi ya Tabata Kisukuru Ephata, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mbunge ataka Chadema ifutwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Temeke (CCM), Abdallah Mtolea, amehoji ni lini hasa Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, atakuwa amejiridhisha kwamba matukio ya fujo na siasa za chuki zinazofanywa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo(Chadema) ni sababu za kutosha kukifuta chama hicho.

Akichangia bungeni jijini hapa jana, hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/21, Mtolea alisema matukio ya fujo na siasa za chuki zinazofanywa na Chadema ni sababu tosha ya kukifuta.

Mbunge huyo ambaye 2015 alishinda ubunge akiwa mwanachama wa CUF chini ya Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) ambao Chadema ilikuwa sehemu yake, alisema mwaka jana Sheria ya Vyama vya Siasa iliboreshwa na kumpa nguvu Msajili kuwa na meno kwenye kuvibana vyama hivyo nchini.

Alisema kutokana na marejeo hayo ya kisheria anaona ni wakati mwafaka kwa Msajili kukifuta chama hicho kutokana na kile alichodai matukio ya fujo na siasa za chuki zinazosababisha mihemko ya chuki zinazofanywa na Chadema.

"Chama hiki kimesababisha fujo nyingi na moja kati ya hizo ni ile iliyofanyika Februari 16, 2018, iliyopelekea kifo cha mwanafunzi ambaye ni binti mdogo Aquilina Aquilini jijini Dar es Salaam,"alisema.

Mbunge huyo alisema hali hiyo ilitokana na chama hicho kukataa amri ya polisi.

"Kibaya zaidi chama hiki hakionyeshi kujutia tukio hili, hukumu ilipotoka ilitegemewa kuwa, kama viongozi wa wananchi wangeenda kuiomba samahani na kuipa pole familia yake, jambo ambalo halikufanyika.

"Wakaanza kufanya vikao na waandishi wa habari vya kisiasa, wakafanya vikao asubuhi, mchana na jioni, wakilia kwa furaha baada ya shauri hilo kuisha, wakati hawa wanalia kwa furaha mama wa marehemu analia kwa uchungu," alisema.

Mtolea alisema mbwebwe za kuchangishana fedha hazikuwa zinafanywa dhidi ya CCM wala serikali, bali zilikuwa zinafanywa dhidi ya Mama Aquilina ambaye amepoteza mtoto.

Mbunge huyo alisema mambo hayo kama Msajili anaendelea kuyaangalia na kuyakalia kimya, vyama vina mwelekeo mbaya.

Alikumbusha kuwa mambo hayo pia yalijitokeza kwenye msiba wa aliyekuwa Mbunge wa Buyungu, Kasuku Bilago, akisema kuwa wakati Bunge na serikali walishirikiana vizuri na familia, lakini Chadema walilazimisha ratiba za mazishi kubadilishwa ili wafanye siasa.

"Tukiendelea kuyavumilia haya, tunatengeneza siasa za aina gani? Ifike mahala Msajili awe mkali, asilichoshe Jeshi la Polisi kufanya vitu ambavyo na yeye pia ana nafasi ya kuvifanya," alisema.

Katika mchango wake, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Hawa Mwaifunga, alimtaka Msajili wa Vyama vya Siasa kutumia nafasi yake vizuri kukemea kauli zisizofaa zinazotolewa na viongozi wa vyama vya siasa bila kubagua.

## Serikali yaanika matumizi mabilioni ya Benki ya Dunia

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesema Dola za Marekani milioni 500 zilizoidhinishwa na Benki ya Dunia (WB) wiki hii kwa ajili ya Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), zitatumika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za sekondari nchini.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati akizungumzia mradi huo na kusema kuwa, watajenga pia miundombinu ya shule, kutoa mafunzo kazini kwa walimu na wanafunzi kuhusu masuala ya kidigitali.

"Serikali imefanya jitihada kubwa ya kuongeza miundombinu katika maeneo mbalimbali ya elimu baada ya mwitikio mzuri wa elimu bila malipo ambao utaongeza idadi kubwa ya wanafunzi wanaokwenda kujiunga na elimu ya sekondari. Mradi huu utasaidia katika kuboresha na kuongeza miundombinu katika shule za sekondari nchini ambazo zitapokea wanafunzi hao waliotokana na mwitikio wa elimu bila malipo," alisema Prof. Ndalichako. Alifafanua kuwa mafunzo kazini yatasaidia kuongeza ujuzi na stadi ambazo zinaendana na wakati ili kufundisha vizuri zaidi na mafunzo ya kidijitali kwa wanafunzi wa shule hizo.

Aidha, alisema mradi huo utajenga mabweni, shule maalum mpya za wasichana zenye mabweni pamoja na kuimarisha utoaji ushauri nasaha ili wanafunzi wanaokutana na changamoto mbalimbali maeneo ya shule, kwenye familia na jamii kwa ujumla wawasilishe hapo na serikali izifanyie kazi kwa urahisi.

"Watoto wa kike wamekuwa wakipata vikwazo kutokana na umbali wa shule na kusababisha kupata changamoto wanapokwenda ama kurudi shuleni kwa hiyo kupitia mradi huu tunakwenda kujenga shule za bweni kwa ajili ya watoto wa kike," alisisitiza Prof. Ndalichako. Ndalichako alisema mradi huo unatarajiwa kuwanufaisha wanafunzi zaidi ya milioni sita na Serikali imefungua milango yake katika kupokea ushauri, maoni na mapendekezo kuhusu namna ya utekelezaji wa mradi huo ili kuwa na manufaa kwa nchi.

# Wakulima michikichi walia kukosa mikopo

**Na Ashton Balaigwa,** KIGOMA

KUKOSEKANA kwa soko la uhakika la mafuta ya mawese kwa wakulima waliounda vyama vya msingi vya Ushirika (Amcos) vinavyojishughulisha na kilimo cha Michikichi katika Mkoa wa Kigoma, kumewasababishia kukosa mikopo kutoka taasisi za fedha kwa ajili ya kuendeleza zao hilo.

Kutokana na hali hiyo, viongozi wa vyama hivyo vinavyofikia 13 kwa sasa wameiangukia serikali ingilie kati, ili wapate mikopo kutoka taasisi hizo kuendeleza kilimo hicho ikiwa ni kutekeleza agizo la Waziri Mkuu kwa vyama hivyo kujikita kwenye kilimo kusaidia upatikanaji wa mafuta ya kula nchini.

Katibu wa Amcos ya Muungano wa Wazalishaji wa Mafuta ya Mawese katika kijiji cha Chakulu, wilayani Uvinza, Moses Malulu, aliwasilisha malalamiko hayo kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Kilimo Tanzania (Tari), Dk. Yohana Budeba, aliyeongozana na Mkurugenzi Mkuu, Dk. Geofrey Mkamilo, waliotembelea ushirika huo ili kujionea maendeleo ya kilimo hicho.

Alisema baada ya kuhamasika kulima kilimo hicho kutokana na kauli ya Waziri Mkuu aliyetembelea Mkoa wa Kigoma na kuwahakikishia watapata mikopo ya kilimo kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania(TADB), waliamua kuungana na kuanzisha ushirika huo na kukamilisha taratibu zote.

Pamoja na kufanya hivyo, lakini mpaka sasa hawajapata mkopo wowote, hivyo kujikuta wakishindwa kujua nini kifanyike.

Alisema waliwasilisha pia ombi hilo la kupata mkopo katika asasi ya kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (PASS) ambao walifika katika mashamba yao na kuwaandikia michanganuo, ili wapate mikopo kwenye taasisi nyingine za kifedha lakini mpaka sasa ombi lao limegonga mwamba.

Naye Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Amcos katika Mkoa wa Kigoma, Hussein Makolokocho, alisema wanashangazwa na taasisi hizo za fedha kushindwa kuwapatia mikopo kwa dhamana ya mashamba ya muungano wa vyama vya ushirika na kumuomba Waziri Mkuu kuingilia kati.

Akizungumza baada ya kuwasilisha ombi hilo, Dk. Budeba, alizipongeza Amcos hizo kwa kutikia agizo la serikali la kuendeleza michikichi kwa kutumia mbegu ya kisasa aina ya Tenera inayozalishwa na taasisi hiyo na kuHidi kulifikisha ombi lao kwenye mamlaka husika. Naye Dk. Mkamilo alisema wamepewa jukumu la kuzalisha mbegu za kutosha za kisasa za michikichi aina ya Tenera ambayo mpaka sasa wamezalisha miche milioni 1.7 na kuwapatia bure wakulima wa mkoa wa Kigoma na lengo lao kufikia miche milioni tano ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

# Corona yamponza Masanja Mkandamizaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Mji wa Dodoma, Patrobas Katambi, amemtaka msanii wa vichekesho nchini, Emmanuel Mgaya, maarufu kama Masanja Mkandamizaji, kuripoti polisi ndani ya siku tatu kutokana na alichodai mzaha aliouonyesha kuhusiana na ugonjwa wa corona.

Masanja alitupia video katika mitandao ya kijamii akihoji watu kuhusiana na ugonjwa huo jijini hapa huku baadhi ya watu aliokuwa akiwahoji wakisema hawaogopi corona na ije tu.

Akizungumza jana jijini hapa, Katambi alisema wakati dunia nzima inahaha kutafuta suluhu ya gonjwa hilo, cha kushangaza Masanja anafanya mzaha, hivyo atatakiwa kwenda polisi kueleza alikuwa anamaanisha nini.

"Nimtake Masanja aje katika Ofisi za Mkuu wa Wilaya hapa Dodoma, atueleze alivyokuwa akifanya mzaha kuhusu gonjwa hilo alikuwa ana maana gani. Watu wanakufa na corona yeye analeta mzaha?" alihoji.

Pia Katambi alisema kama Rais John Magufuli alichukulia uzito mkubwa tatizo hilo nchini na kutoa tahadhari kwa wananchi, huyo Masanja ni nani mpaka anapingana naye.

Katambi alisema Waziri Mkuu aliunda kamati za kukabiliana na ugonjwa huo ambazo bado zinaendelea na mikakati ya kuzuia corona na kupambana lakini cha kushangaza anatokea mtu anaamua kupotosha, jambo ambalo si jema.

Alisema Masanja alifanya tukio hilo akiwa jijini hapa kwa kutumia neno la Kiingereza la Covid-19, akitaka kuonyesha wananchi wa Dodoma hawana uelewa wa ugonjwa huo.

"Kama dunia nzima inapambana yeye anataka kuonyesha dunia kuwa wakazi wa Dodoma hawana uelewa wa tatizo hilo?" alihoji.

Dunia nzima ikiwamo Tanzania, inaendelea na mapambano dhidi ya corona huku wanasayansi nguli wakiendelea kuhaha kutafuta chanjo ya ugonjwa huo ambao unaua kwa haraka.

Mpaka sasa kuna wagonjwa 20 ambao wamethibitika kuwa na maambukuzi ya virusi vya Covid 19 ndani ya Tanzania huku watu 273 Tanzania Bara na Zanzibar ni 30 walichukuliwa sampuli za kupima virusi vya corona.

Aidha, washukiwa wa virusi vya corona wamewekwa karantini ya lazima kwa siku 14 katika maeneo maalumu yaliyobainishwa na serikali kwa gharama zao.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kushoto), akitoa elimu ya ulipaji kodi ya ardhi kwa hiari kwa Mkurugenzi wa gereji ya Mwananchi, Polycapy Kimario (kulia), ambaye anadaiwa kodi ya ardhi Sh. milioni tisa, wilayani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Jela miaka 30 kwa kubaka mwanafunzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi, imemhukumu mkazi wa Kata ya Kiwalala, wilayani hapa, Zacharia Kasuka (30), kifungo cha miaka 30 jela na kulipa fidia ya Sh. 500,000 baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mwanafunzi wa shule ya sekondari mwenye umri wa miaka 16.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi Muyoga Magala, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri.

Baada ya kutiwa hatiani, mshitakiwa aliulizwa iwapo anazo sababu za msingi zitakazoishawishi mahakama isimpe adhabu kali kutokana na kosa linalomkabili na kuomba aonewe huruma kwa kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza.

Aidha, alidai kwamba alijikuta akishiriki kimapenzi na mwanafunzi huyo wa baada ya kutingwa na ibilisi wa mapenzi.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Rabia Ramadhani, aliomba mahakama kumpa adhabu kali mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia ya kupenda kuchukua watoto wadogo na wanafunzi na kuwasababishia kukatisha masomo na ndoto zao za baadaye.

Hakimu Magala akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 87/2019, kupitia vifungu vya Sheria 130 (1) (2) (e) na 131 (1) vya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marejea mwaka 2002, alisema amepokea maombi ya pande zote mbili lakini kutokana na sheria kumfunga mikono, akamhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani na atakapomaliza amlipe mlalamikaji fidia ya Sh, 500,000.

Awali ilidaiwa na mwanasheria wa serikali kuwa mshtakiwa alikamatwa Novemba 26, mwaka jana na wazazi wa mwanafunzi walioshirikiana na askari polisi akiwa na mwanafunzi huyo nyumbani kwake.

Mwanasheria huyo alidai mahakamani kuwa mshtakiwa alifanya kosa hilo akiwa amepewa kazi ya kuhudumia shamba la wazazi wa mwanafunzi huyo.



Ofisa Afya wa Kituo cha Forodha cha Namanga, mkoani Arusha, Dk.Gabriel Mdachi (wa pili kushoto), akitoa maelezo ya udhibiti wa virusi vya ugonjwa wa Corona kwa baadhi ya Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, walipotembelea kituo hicho, juzi. Kushoto ni Mbunge wa Bunge hilo, Fancy Nkuy na (kulia) ni Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Kituo cha Namanga, Paul Kamkulu. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Mkurugenzi afanya ziara kukagua vitakasa mikono

**Na Allan Isack,** BABATI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Hamisi Malinga, kwa kushirikiana na maofisa afya wa eneo hilo, wamefanya ukaguzi wa matumizi ya vitakasa mikono kwa wananchi kwa lengo la kupambana na maambukizi ya virusi vya corona.

Malinga alifanya ukaguzi huo ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti.

Mnyeti alitoa agizo kwa viongozi wa serikali mkoani hapa kuhakikisha vitakasa mikono vinapatikana na kusambazwa katika maeneo yote hususani kwenye mikusanyiko ya watu.

Malinga na timu yake walitekeleza agizo hilo, kwa kutembelea minada ya Dareda na Ayalagaya na kutoa elimu ya kujinga na maambukizi ya corona kwa wafanyabiashara na wateja katika maeneo ya minada. Aliwataka wafanyabiashara hao, kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono kwa maji yanayotiririka kuepuka kusalimiana kwa kushikana mikono, kuziba mdomo kwa kutumia viungio vya mkono wakati wa kupiga chafya.

Licha ya kuzungumza hayo, aliwataka wafanyabiashara hao kutumia vitakatisha mikono ili kujikinga na ugonjwa huo kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba.

"Ndugu zangu wafanyabiashara na wateja wa eneo hili, hakikisheni mnazingatia hatua zote zinazotakiwa kuchukuliwa ili kujikinga na janga hili la corona," alisema Malinga.

Akizungumzia malalamiko ya vitakasa mikono kupanda bei, aliwahakikishia wananchi kuwa serikali ya mkoa kwa kushirikiana na kiwanda cha Mati Super Brands kilichoko Babati Mjini, watahakikisha bidhaa hizo zinapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu katika maeneo yote ya minada na makazi ya watu.

Alisema viongozi wa kiwanda hicho, wamewahakikishia bidhaa hizo, zitazalishwa za kutosha na zitauzwa kwa bei ambayo kila mwananchi atamudu kununua. Naye Meneja Masoko wa Mati Super Brands, Aloyce Mvungi, alisema wametengeneza vitakasa mikono kwa kila ujazo na bei tofauti kulingana na kipato cha Mtanzania wa kawaida.

Mvungi alisema bei ya kiwandani ya bidhaa hizo ni kuanzia Sh. 1,500 hadi Sh. 12,500 kutegemeana na ujazo.

Ofisa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Suten Mwabulambo, aliwataka wafanyabiashara mnadani hapo, kutumia elimu watakayopewa kufikishia ujumbe kwa wananchi wengine kwenye minada mbalimbali, pamoja na nyumbani kwao kwenye familia zao.

"Nawashauri ndugu zangu hakikisheni mnaitumia elimu mtakayoipata hapa, kufikishia kwa wengine kwenye minada mnapozunguka na hata majumbani kwenu," alisema.

Mwenyekiti wa Minada, Khalifa Ally, aliwataka wafanyabiashara hao kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu ili kujikinga na maambukizi ya corona. Aliwahakikishia wataalamu hao kuwa wamejitahidi kuweka ndoo za kunawia mikono kila sehemu ya mnada pamoja na kuweka jeshi la akiba ili kuwalazimisha wananchi kunawa mikono waingiapo na kutoka mnadani hapo.

# Watahadharishwa migogoro ndoa kwa malezi ya watoto

**Na Allan Isack,** BABATI

MSHAURI wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto kutoka shirika la Children in Crossfire la Ireland ya Kaskazini, Davis Gisuka, amewatahadharisha wanandoa wenye migogoro kuacha kwa kuwa inasababisha matatizo kwa watoto wadogo.

Tahadhari hiyo aliitoa wakati akizungumzia namna migogoro ya wanandoa inavyoathiri malezi na ukuaji wa watoto wadogo.

Sambamba na hilo, alitoa wito kwa jamii kuhakikisha migogoro ya familia zao wanaitatua bila kuleta madhara kwa watu wengine.

Wakili wa Kujitegemea, Nickson Maganya, alisema Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, sura ya 29 imezungumzia namna ya kuwasaidia watoto endapo ikitokea wazazi wao wameachana.

Mwanasheria huyo alisema pindi migogoro hiyo inapotokea kwa wanandoa, madhara yanawakuta watoto kukosa malezi ya baba na mama kitu ambacho ni muhimu kuliko vyote kwa wakati huo.

"Mtoto anaweza kukosa elimu kutokana na mgogoro ambao umesababisha familia kusambaratika, hivyo watoto mara nyingi wanajikuta wakiishi katika mazingira magumu na wakati mwingine wanapelekwa kulelewa na watu ambao hawahitaji kuishi nao," alisema Muganya.

Aidha alisema sheria inaeleza kuwa wanandoa wanapotengana mahakama inapaswa kuzingatia maslahi ya watoto ikiwa wana umri chini ya miaka saba.

"Nashauri wanandoa wavumiliane na kuacha tabia zitakazosababisha migogoro kwenye familia zao, kwa kuwa kuachana kunatokana na mambo yao binafsi, na hiyo siyo njia ya kutatua tatizo," aliongeza Muganya. Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Babati, Mathias Focus, alisema kila robo ya mwaka wa fedha, ofisi yake imekuwa ikipokea migogoro ya ndoa kati ya 20 na 50. Focus alisema migogoro mingi ya ndoa inatokea kipindi cha njaa kwa kuwa wanaume wengi wanatelekeza familia zao, kutokana na ugumu wa maisha.

Pia alisema hata kipindi cha msimu wa mavuno yakiwa vizuri migogoro hiyo, bado inakuwapo kutokana na baadhi ya wanaume kuvuna mazao na kuuza halafu wanakwenda kuoa mke wa pili.

# Wanawake waanzisha mradi wa umwagiliaji

**Na Cynthia Mwilolezi,** HANANG'

WANAWAKE 45 katika kijiji cha Mureru, Kata ya Balangdalalu, Hanang' mkoani Manyara, wameanzishiwa mradi wa kilimo cha umwagiliaji na Shirika la Oxfam Tanzania, kwa kushirikiana na Ujamaa Community Resource (UCRT) ili kuondokana na utegemezi kwa wanaume zao na kujikwamua kiuchumi.

Wakieleza juzi manufaa ya mradi huo kwao, baadhi ya wanawake hao, Anneth Gwandu, Monica Barhe na Felista Giyam, walisema mradi huo utawafanya kutokuonekana mizigo ndani ya familia na kwa jamii kwa ujumla.

Pia walisema utaleta mtazamo mwingine mpya na chanya miongoni mwa jamii wilayani hapa, kutokana na jamii ziishio Hanang' kutokumpa nafasi mwanamke.

"Huu mradi kwa kweli kwanza tunawashukuru Oxfam na UCRT kwa kutuletea mradi huu. Mradi huu utatukwamua sana kiuchumi na hata kusaidia baadhi ya majukumu kwenye familia zetu," alisema Felista Giyam ambaye ni mweka hazina wa kikundi hicho.

Alisema pamoja na mradi huo kulenga wanawake ndani yake, kuna wanaume 12 ambao wameamua kushirikiana nao.

Mmoja wa mwanakikundi, Anna Iselu, aliiomba serikali kuwatafutia soko la mazao kwa kuwa wamekuwa wakilima kwa muda mrefu, lakini wanakosa soko, hivyo baadhi yao kukata tamaa kuendelea na kilimo.

"Unajua hapa tunatumia gharama kubwa wakati wa kununua pembejeo lakini tunakosa soko. Jambo hili linaturudisha nyuma kwa kweli, tunaomba serikali iangalie jinsi ya kutusaidia wakulima hasa sisi wanawake," alisema Iselu.

Charles Kidaguwi ni kati ya wanaume ambao wameshiriki katika mradi huo, alisema kwake kuna manufaa makubwa, kwani utamsaidia kuwajibika vyema katika familia tofauti na awali ilikua tegemeo peke ake la kipato.

"Lakini sasa nitasaidiana na mke wangu kutafuta kipato na maisha yatakwenda safi, kwani naamini penye ushirikiano hapakosi heri na naomba wanaume wenzangu washirikiane na wake zao kubuni vyanzo vya kipato na msiwakataze kufanya kazi,"alisema.

Donath Fungu Meneja wa Miradi wa Oxfam Kanda ya Kaskazini, alisema mradi huo wanaufanya kwa kuwashirikisha wanawake na vijana, lengo likiwa ni kuwajengea wanawake uwezo kiuchumi.

Fungu alisema mwanamke atakapopata nguvu ya kuinuka kiuchumi, atapata nafasi ya kufanya uamuzi katika ngazi ya familia, Kijiji hadi ngazi ya kitaifa.



Wasichana waliokimbia ukeketaji, wanaolelewa na nyumba salama ya shirika lisilo la kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania la mjini Mugumu, Serengeti mkoani Mara, wakifanya usafi kwenye barabara inayoelekea kwenye ofisi za shirika hilo, juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Taasisi yajitoa kupambana na corona

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TAASISI ya Maendeleo ya Uru (UDF), imesema inaandaa utaratibu maalum wa kupita kijiji kwa kijiji katika kata 16 za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, kuzungumza na wananchi kuhusu tishio la virusi vya Corona linaloitesa dunia kwa sasa. Mkurugenzi wa Mtendaji wa UDF, Wakili Wilhard Kitali, alisema wakati serikali inaendelea kufanya tathmini ili kuhakikisha inazuia ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (Covid 19) kusambaa kwa kiasi kikubwa nchini, wao wamejipanga kuanza kutoa elimu hiyo kwa wakazi wa Moshi.

"Muda mfupi ujao tutazunguka vijiji vyote Moshi DC (Halmashauri ya Wilaya ya Moshi) kutoa elimu kwa wananchi wa kada zote na ikiwezekana kama tutapata fungu kutoka kwa wahisani tutagawa vitakasa mikono kwa wananchi hao ili kujikinga na ugonjwa huo," alisema Kitali.

Wiki iliyopita, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alielekeza kinga dhidi ya virusi vya corona liwe ni jambo la kimkakati zaidi kuliko kusubiri kutibu. Alisema kwa sasa serikali imeweka mkazo kwenye kuwahamasisha wananchi kujikinga na virusi hivyo.

Kabla ya kutangaza jana kuanza mpango huo, taasisi hiyo ilikuwa imejikita katika shule za sekondari kutoa elimu ya afya ya uzazi hasa hedhi salama na matumizi ya taulo za kike.

Pia, kwa sasa taasisi hiyo inatekeleza kampeni maalum ya kimkakati ya 'Binti Nabaki Darasani.' Kampeni hiyo imepewa jukumu la kutafuta fedha za ununuzi wa taulo za kike kwa ajili ya kuwafikia wanafunzi zaidi ya 4,000 wanaosoma Shule za Sekondari Wilaya ya Moshi.

# Wachukua hatua kupambana na uharibifu wa mazingira

**Na Godfey Mushi,** HAI

WAKAZI wa Kijiji cha Mbatakero, Hai mkoani Kilimanjaro, wameanza kuchukua hatua za kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaochangiwa na ukataji miti kwa ajili ya ujenzi na nishati ya kuni na mkaa.

Hatua walizochukua kuzuia kuendelea kwa uharibifu huo wa mazingira ni pamoja na kuelekeza wakazi wake, kwa kila familia moja kuwa na jiko banifu.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Matumizi Endelevu ya Ardhi (SLM) wa Wilaya ya Hai, Zephania Gunda, ili kuongeza ari ya wananchi kujielekeza katika matumizi ya teknolojia hiyo, halmashauri ya wilaya hiyo imetoa motisha ya majiko banifu 19 yanayohamishika kwa wananchi wa kijiji hicho.

"Nia yetu ni kuhakikisha tunakabiliana vilivyo na uharibifu wa mazingira katika wilaya yetu. Matumizi ya majiko banifu ambayo sifa yake kuu ni kutumia kuni chache, yamewanufaisha zaidi wanawake ambao kwa sasa wanapata muda wa kuendelea na shughuli nyingine za uzalishaji tofauti na awali walipokuwa wakilazimika kutumia muda mwingi kwenda kutafuta kuni.

"Lakini si kuwapunguzia adha pekee ya kwenda kutafuta kuni, bali matumizi ya majiko banifu kwa wanawake yamekuwa tiba ya macho. Wengi wao wamekuwa wakiathiriwa na moshi hata pale ambapo walilazimika kutumia magunzi kupika."

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Juliana Abraham, alieleza furaha yake akisema: "Kweli kwa sasa tunasema asante Mungu kwa sababu hata macho yetu yamepona kwa sababu majiko haya hayatoi moshi kabisa. Tutazungumza na akina baba kila kaya kutengeneza majumbani majiko haya."

Mkazi mwingine wa kijiji hicho, Ibrahim Juma, alisema kijiji hicho ni miongoni mwa maeneo ya tambarare ya Wilaya ya Hai ambayo yameathiriwa kwa kiasi kikubwa na ukataji wa miti kwa ajili ya kuandaa mashamba, ujenzi wa makazi ya muda na uchomaji wa mkaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Yohana Sintoo, akizungumzia mpango huo, alisema baada ya kuanza kufanya wajibu wake, tayari yako matokeo chanya yaliyoanza kuonekana hususani kwenye suala la uchomaji mkaa na ukataji kuni.

Alisema matokeo yaliyoanza kuonekana ni pamoja na wananchi walio wengi kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kutumia majiko banifu yanayotumia kuni chache.

## Msako mkali wakaidi corona

**Na Godfrey Mushi,** SAME

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Same, imeamua kufanya vikao kila baada ya siku mbili kujadili namna ya kuwabana watu wanaokaidi maagizo ya kujikinga na maambukizi ya corona.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Josephine Senyamule, alisema hayo jana wakati akizungumzia mkakati wa kujilinda na homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya ugonjwa huo.

"Kwanza tumeiteua Zahanati ya Ishinde kuwa ndicho kituo chetu cha kupokea washukiwa wa corona lakini pia tumeweka utaratibu wetu wa kiserikali kwamba ni lazima kamati ya ulinzi na usalama ikutane kila baada ya siku mbili.

"Hivi sasa tunapita katika masoko, maeneo ya starehe na maeneo yote yanayovutia watu kuweka mikusanyiko kila siku, kuangalia kama kuna watoto wanaachwa kuzurura mitaani lakini pia ambao wanapuuza maelekezo ya serikali hasa matumizi ya vitakasa mikono na kuweka maji na sabuni kila eneo," alisema.

Kuhusu watoto wanaozurura mitaani au kucheza nje ya makazi yao, Senyamule ameagiza watendaji wa vijiji na wenyeviti wa vitongoji kuzionya familia hizo lakini pia kuchukua hatua ya kuwazuia watoto kuonekana katika mikusanyiko.

Katika wilaya hiyo, bado baadhi ya kaya hazichukui tahadhari ya kuwazuia watoto kuzurura mitaani ili kujikinga na ugonjwa huo.

Ugonjwa huo wa homa kali ya mapafu, unasababishwa na kirusi jamii ya corona (Covid 19) ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov Corona Virus mwaka 2013.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo. Dalili za ugonjwa huo huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.



# Wagonjwa wakwama kwenda hospitalini

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

WAKAZI wa vijiji vya kata ya Mvumi Misheni, Chamwino mkoani Dodoma, wakiwamo wajawazito wameshindwa kupata huduma za afya kutokana na daraja linalounganisha eneo hilo na hospitali kusombwa na maji ya mvua.

Kutokana na hali hiyo, wakazi hao wamelazimika kutumia nguvu kazi na kuchangishana fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo ambalo pia magari na mizigo mingine ilikwama kwa zaidi ya siku mbili.

Kutokana na adha hiyo, wananchi hao wameiomba serikali kuwajengea madaraja kwenye eneo hilo ili kuwawezesha wananchi na magari kupita kwa urahisi muda wote tofauti na ilivyo hivi sasa wanavyopita kwa shida wakati mvua zikiendelea kunyesha.

Helena Mahembe, akizungumza kwa niaba ya wakazi hao kwenye eneo hilo la daraja juzi, aliiomba serikali kuangalia kwa jicho la upana kwenye eneo hilo kutokana na shida kubwa wanayokabiliana nayo katika kipindi hiki cha mvua.

"Maji yakijaa kwenye eneo hili hakuna gari lolote linaloweza kupita zaidi ya pikipiki. Hali hii kuna hatari siku nyingine wajawazito wanaweza kujifungulia hapa na wakakosa msaada kutoka kwa wahudumu wa afya" alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Alfa Nzoya, alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo kwenye maeneo hayo ya madaraja yaliyopo karibu na makaburi katika barabara inayounganisha Mvumi Misheni na Dodoma mjini.

Alisema eneo hilo ni la mkondo wa maji yanayotoka milimani, hivyo kuna kila sababu kwa serikali kutumia jitihada zake za kufanya ukarabati wa madaraja ili kupitika kwa msimu wote.

Naye Diwani wa Mvumi Misheni, Matalamla Masaka, aliwashukuru wananchi hao kwa kushirikiana kwa pamoja kwa kufanya ukarabati na kuwezesha huduma ya usafiri kurejea.

Alisema kuwa, mbali na kutumia nguvu kazi pia wananchi hao wamechanga fedha taslimu kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kama vile mifuko ya saruji.

# Wahadharishwa kuhusu viongozi matapeli

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wadogo wadogo, wakiwamo mama lishe wametakiwa kujihadhari na viongozi wanaojihusisha na uuzaji wa maeneo ya kufanyia biasahara yaliyoko katika stendi za mabasi na masoko kwa kuwa wengi wao ni matapeli.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, wakati akizungumza na wafanyabiashara hao.

Yuna alisema wenye mamlaka ya kutoa vibali vya kuuza na kuwaweka maeneo ya kufanya biashara kama vile kwenye stendi ya daladala na masoko ni halmashauri ya jiji pekee na si vinginevyo. Aidha, alisema walengwa wa tahadhari hiyo ni wafanyabiashara wadogo wadogo wakiwamo mama lishe waliojenga mabanda yao kwenye maeneo yasiyo rasmi katika stendi za daladala, masoko, barabarani na mengine yasiyoruhusiwa.

Ofisa huyo ambaye alifanya ziara ya kushtukiza kwenye stendi ya mnanda mpya ulioko Kizota, aliwataka wafanyabiashara hao pamoja na mama lishe kujihadhari na viongozi wanaowasimamia kwenye maeneo yao ambao si waaminifu. Alisema viongozi wengi wamekuwa na tabia ya kudai kuwa wametumwa na wana vibali vinavyoweza kuwapatia maeneo ya kufanya biashara huku wakiwataka kutoa fedha.

"Naomba nyie mama lishe na wamachinga toeni taarifa pindi viongozi wenu wanapowaomba rushwa ili mpatiwe maeneo, mkikaa kimya mtabakia kulalamika pale utakapotakiwa kuondolewa na jiji," alisema.

Baadhi ya wafanyabiashara na mama lishe walioko kwenye maeneo hayo yasiyo rasmi, walidai kuuziwa na viongozi wao huku wakiwatumainisha kuwa halmashauri ya jiji haitawaondoa.

Halima Abdalah, mama lishe wa stendi mpya ya Kizota, alisema ili kupata eneo la kuuza chakula au kufanya biashara ni lazima uuziwe na viongozi ambao wanadai kuwa Halmashauri ya Jiji hawatawaondoa.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mbuyuni, Kata ya Kizota, Mikidadi Abdallah, akizungumza na wafanyabiashara hao, alikiri kupokea malalamiko ya kuuziwa maeneo hayo.

Hata hivyo, aliwataka kutoa taarifa pindi wanapoombwa fedha ili wapatiwe maeneo ya biashara kwa kuwa sehemu walipo si rasmi kwa ajili ya kufanya biashara yoyote.

Diwani wa Kizota, Gerald Paulo, aliwataka wafanyabiashara kuheshimu na kutii sheria na kanuni za Halmashauri ya Jiji hususani zile zinazokataza kufanya biashara maeneo yasiyo rasmi.



Wananchi wa Kata ya Mvumi Mission, Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma, wakisukuma gari la mizigo namba T263CJU Fuso, lililokwama kwenye eneo la mkondo wa maji, karibu ya makaburi ya Mvumi, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Matumizi ya magogo kwa ukataji nyama yapungua

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Nyama imesema utumiaji wa magogo katika bucha kwa ajili ya kukatia nyama, umepungua kwa kiasi kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali.

Bodi hiyo, chini ya Kaimu Msajili Imani Sichalwe, ilifanya ziara ya kushtukiza katika bucha zilizoko katika soko la Majengo jijini Dodoma kwa wafanyabiashara ambao bado wanatumia magogo kukata nyama na kubaini wengi wao wanatumia misumeno ya mashine.

Alisema katika ziara ya awali walitoa agizo la watu kuacha mara moja matumizi ya magogo hayo.

Ziara hiyo imefanyika kutokana na katazo la matumizi ya magogo ifikapo Septemba 9, mwaka jana huku wakitakiwa kutumia mashine za umeme au kifaa maalumu ambacho ni mbadala wa magogo hayo.

Akizungumza na wafanyabiashara hao baada ya ukaguzi, Sichalwe alisema magogo hayo ni machafu kutokana na kuhifadhi uchafu kwa muda mrefu ambao unaweza kutengeneza vijidudu vitakavyosababisha magonjwa ya kuhara, hivyo ni hatari kwa afya za walaji.

"Hata nyinyi waandishi wa habari mmeona uchafu wa muda mrefu uliotoka kwenye lile gogo nililolikwangua na kisu. ndivyo hivyo uchafu ule unabaki kwenye nyama na mlaji asipoosha vizuri na kuichemsha husababisha magonjwa kama kuhara na mengineyo," alisema Sichalwe.


Aliongeza kuwa utumiaji wa mapanga na mashoka katika kukata nyama si salama kwa kuwa chembechembe za mifupa zinabaki kwenye nyama na endapo mlaji atakula husababisha kansa na kidole tumbo (appendix).

Naye Mshauri wa Mifugo wa Mkoa wa Dodoma, Goodluck Ndaweka, alisema changamoto zilizopo kwa wafanyabiashara hao ni ndogo ndogo na zinarekebishika, hivyo aliwashauri kuzitatua ili kuwapatia wateja wao huduma safi na salama.

"Mkifuata taratibu na sheria hakutakuwa na tatizo lolote kwenu na pia mtafanya kazi kwa uhuru wakati huo huo mkiwapatia wateja huduma inayostahili kwa vigezo vyote," alisema Ndaweka.

Akizungumza kwa niaba ya wamiliki wa bucha, Charles Laizer, alisema endapo wataondolewa magogo watapata taabu katika ukataji wa nyama kwa kuwa mashine haiwezi kukata nyama kubwa, hivyo ni lazima wapatiwe mbadala wa magogo na pia kifaa hicho lazima kiwe na uwezo wa kustahimili ukataji wa nyama.

"Nyama zingine ni kubwa sana haziwezi kukatwa kwa mashine na kama kuna mbadala basi ukate nyama na iwe na uwezo kama wa gogo kwani gogo linasaidia sana katika ukataji wa nyama haswa kubwa. Lakini pia muda mwingine kunakuwa hakuna umeme hivyo tunaomba serikali ilitazame hili kwa jicho la tatu," alisema.





Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mwakilishi Simai Mohamed Said (kulia), akikabidhi msaada wa vifaa vya ujenzi wa maktaba kwa shule ya Kibele, Tunguu, Mkoa wa Kusini Unguja jana. Kushoto ni Diwani wa wadi ya Ubago, Ali Mtumwa.
**PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Wafanyabiashara watoa msaada kupambana na virusi vya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Wazalendo wa Wafanyabiashara katika kupambana na corona, umeikabidhi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) vifaa na vitu mbalimbali kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo.

Vifaa hivyo ni pamoja na dawa za kuosha mikono, masksi, matangi ya kuhifadhia maji, sabuni na vyakula kama vile sukari, mchele, unga wa ngano na mafuta ya kupikia vyenye thamani ya Sh. milioni 100.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud, alisema vifaa hivyo vitatumika kama ilivyokusudiwa.

Waziri alisema endapo mtumishi yeyote wa serikali atakayevitumia vifaa hivyo kinyume cha utaratibu kwa kujinufaisha, atafukuzwa kazi.

"Napenda kuwaeleza kuwa vifaa hivi vimekuja muda mwafaka na vitatumika kama ilivyokusudiwa na yeyote atakayevitumia kinyume hana kazi " alisema Aboud.

Pia alisema hakuna mwenyewe uhakika wa usalama dhidi ya corona, hivyo ni vyema kila mmoja akachukua tahadhari ya kujikinga .

Sambamba na hilo, aliwataka wananchi kufuata maelekezo ya Wizara ya Afya katika kujikinga na ugonjwa huo ili afya zao ziwe bora huku akisisitiza kuwa ugonjwa huo ni hatari kwa afya za wananchi, uchumi na maisha ya jamii.

"Tunapambana na vidudu tusivyovijua, hivyo ni vyema kushirikiana namna ya kuepukana na virusi hivyo," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Wazalendo na Wafanyabiashara, Abdulsamad Abdulrahim, alisema kasi ya kupambana na ugonjwa huo inazidi kuongezeka.

Alisema katika kuunga mkono jitihada za serikali kupambana na ugonjwa huo, wameamua kutoa msaada huo ili kuhakikisha mapambano ya dhidi ya ugonjwa huo yanaleta ushindi.

Naye Naibu Waziri wa Afya, Harusi Suleiman, alisema wananchi wamekuwa na hofu kutokana na ugonjwa wa corona, hivyo ni vyema kushirikiana kuutokomeza.

"Kutoa ni moyo si utajiri tunawapongeza sana kwa msaada huu na tunawaahidi kuwa utatumika sehemu zinazohitajika," alisema.

# Madereva watakiwa kufuata utaratibu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mustafa Aboud Jumbe, amezitaka jumuiya za magari ya abiria kufuata utaratibu uliowekwa na Wizara ya Afya kwa lengo la kuepuka maambukizi ya maradhi ya corona.

Hayo aliyasema jana katika Ukumbi wa Bodi ya Usafiri Barabarani, Mwanakwerekwe, wakati wa kikao cha Idara ya Leseni na Jumuiya za Magari ya Abiria kwa mikoa mitatu ya Unguja. Alisema ni vyema kwa madereva na makondakta kufuata masharti yaliyowekwa na Wizara ya Afya ili kudhibiti kuenea kwa janga hilo.

"Ni vyema kufuata masharti yaliyowekwa na wataalamu kwani maradhi hayo si ya kuyafanyia mzaha hata kidogo," alisema.

Pia aliwataka viongozi wa jumuiya kushirikiana na serikali kuhakikisha wanachukua tahadhari kwa vyombo vya usafiri kwa abiria wanaotumia usafiri wa nchi kavu ili kudhibiti kuenea kwa maradhi hayo.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Zanzibar, Kamishna Msaidizi (ACP) Robert Hussein, aliwataka madereva na makondakta wa magari ya abiria kufuata maelekezo yanayotolewa na jeshi la polisi kwa kuwa kwenda kinyume ni kosa kisheria.

Alisema Jeshi la Polisi litamchukulia hatua dereva na kondakta atakayebainika anavunja sheria na kuwahakikishia kuwa hatua zitachukuliwa papo hapo.

Miongoni mwa maazimio ya kikao hicho ni pamoja na kuwataka wakuu wa jumuiya kuhakikisha kila gari linachukua abiria kwa idadi waliyoruhusiwa.

# ...Waziri ataka nguvu ya pamoja dhidi ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wa Mkoa wa Kusini Unguja, wakiwamo madereva wa gari, wametakiwa kuchukuwa tahadhari kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona ambao ni janga la kimataifa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema hayo wakati akikabidhi vifaa mbalimbali kwa ajili ya kinga dhidi ya corona vikiwamo vitakasa mikono, sabuni na ndoo za kuhifadhi maji kwa ajili ya kunawa mikono.

Alisema njia sahihi za kuepukana na corona ni kwa wananchi kufuata masharti yanayotolewa na wataalamu wa afya ikiwamo kuepuka mikusanyiko ya watu katika maeneo mbalimbali.

Suleiman alisema serikali zote mbili zimechukuwa hatua za tahadhari kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa huo ikiwamo kufunga shule zote kuanzia za msingi, sekondari hadi vyuo vikuu.

Alisema lengo la hatua hizo ni kuwaepusha wananchi dhidi ya kuenea kwa corona, ugonjwa ambao hadi sasa umeathiri karibu nchi zote duniani.

"Njia nzuri za kuepukana na ugonjwa wa corona ni wananchi kufuata masharti yanayotolewa na wataalamu wa afya, ikiwemo kujiepusha na mikusanyiko mikubwa ya watu katika maeneo mbalimbali. Watu wakiona dalili za ugonjwa huo wafike katika vituo vya afya kwa ajili ya uchunguzi," alisema.

Pia aliwataka viongozi wa dini kuendelea kuliombea taifa dua katika kipindi cha ibada katika misikiti mbalimbali huku waumini wakitakiwa kuongeza ibada zaidi.


"Hiki ni kipindi kizuri ambapo waumini wa dini mbalimbali wanatakiwa kuongeza muda wa kufanya ibada kwa ajili ya kumwomba Mwenyezi Mungu kutuepushia janga hili la corona," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Idrissa Kitwana, alisema elimu inaendelea kutolewa kwa wananchi wa jimbo la Makunduchi katika kujikinga na corona.

"Kwa muda wa mwezi sasa tunatoa elimu juu ya ugonjwa wa corona katika makundi mbalimbali wakiwamo madereva na wamiliki wa hoteli huku tukiwataka wananchi kutoa taarifa wakati wanapomwona mgeni," alisema.

Sheha wa Muyuni A Unguja, Maulidi Hassan Zidi, alisema atahakikisha vifaa hivyo vinawafikia wananchi wa shehia yake kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

"Tunamshuru mwakilishi wetu pamoja na mbunge kwa kutufikishia vifaa hivi ambapo tunaahidi vitawafikia walengwa," alisema.




**AMBER LULU**

Soma UK.14

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI APRILI 4, 2020



# ANAPOTEA VANESSA MDEE ATAHADHARISHWA

Soma UK.16

## BASI SAWA




# Pablo ainogesha 'Koti la Kuazima' Phantom Musica

MWIMBAJI Pablo Masai ni kati ya waimbaji walioshiriki kwenye kibao kipya cha kundi la Phantom Musica International kinachojulikana kwa jina la'Koti la Kuazima'.


Wimbo huo kwa sasa upo katika orodha ya kazi mpya za muziki wa dansi zinazosikika kupitia vituo vya redio na mitandao ya kijamii.

Akitambulisha wimbo huo, Abdulfareed Hussein ambaye ni Mkurugenzi wa kundi hilo, amesema Pablo Masai ameongeza vionjo vipya katika wimbo huo.

Amesema Phantom Musica International iliamua kumshirikisha Pablo kama sehemu ya kuongeza 'utamu' katika safu ya waimbaji wa kibao 'Koti la Kuazima'.

"Ni mpango kazi wa kundi letu kuwashirikisha wanamuziki mbalimbali katika kila kazi na safari hii tumeongeza sauti ya mwimbaji huyo na amefanya kazi kisawasawa" alisema Abdulfareed.

Alizitaja nyimbo tano ambazo zimekamilika ni 'Sononeko la Huba. Sekidobwa, Nanawa Mikono na Sitobadilika.



# Amber Lulu jitahidi utampata mume

MSANII wa Bongo Fleva, Amber Lulu, amesema anatamani kumiliki mume wake ili hata siku akimposti katika mitandao ya kijamii amuite kwa mahaba.

Amber Lulu ameweka wazi hilo kupitia ukurasa wake wa Instagram ambapo ameandika.

"Mimi natamani kuwa na mume wangu mwenyewe, ambaye hata nikimpost kama Queen Darleen na mimi aniite mke wangu, ila sisi wengine tuna nyota ya kuwa michepuko" ameandika Amber Lulu.

Katika maisha yake ya uhusiano wa kimapenzi, msanii huyo alikuwa na Young Dee pamoja na Prezzo kutoka nchini Kenya.



# CHIDI BENZ SIJUI KAMA HARMONIZE ATAKUELEWA

RAPA mkongwe nchini, Chidi Benz, amempa sharti msanii mwenzake Harmonize, kukubali kuandikiwa wimbo kama akitaka kufanya kazi pamoja.

Chid Benz amesema sasa hivi hana ukaribu na Harmonize zaidi ya kazi pekee, na mara ya mwisho kuonana naye ilikuwa katika uzinduzi wa Album yake ya Afro East , Machi 13, mwaka huu.

"Nipo karibu sana na Harmonize kama msanii, ila sipo kama watu wanavyoongelea, sijawahi kufanya naye kazi na sio mbaya kama nitafanya naye. Akae akijua akitaka kufanya wimbo na mimi lazima nimuandikie, nimpe wazo na nimtafutie mdundo, kama akiona mbaya basi ataandika ya kwake " ameeleza Chidi Benz.

## INSTA-TWITTER





**Halafu** nimesahau. Kuhusu kufunika nywele jamani mtanisamehe maana hata nikiwa napikia ndugu, jamaa na rafiki sifunikagi nywele. Je, wewe unafunikaga nywele ukiwa home? Tukimaliza tunakula wenyewe na watu wanaotuzunguka. Tukila nywele zetu wenyewe sio mbaya. Mtu nimedamshi, hivyo uende ukanitie na mkofia jamani? Hapana wapenzi wangu nitashindwa-**Wema Sepetu.**



**Nimeamini** mtoto wa msanii naye pia ni msanii. Huyu mtoto wangu Mwinshehe Kingwendu anajifanya yuko Sauzi kumbe yuko Mbagala-**Kingwendu.**



## Nay wa Mitego wakati mwingine busara zimejaa

KATIKA mitandao ya kijamii kumetawala gumzo la mfanyabiashara Chiddi Mapenzi, kumuandikia ujumbe wa kumkumbuka aliyekuwa mkewe Shamsa Ford na kujutia kumpoteza.

Hata hivyo, rapa Nay Wa Mitego, ameingilia kati kwa kumuomba Shamsa amsamehe mumewe na kurudiana naye.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Nay Wa Mitego ameandika , "Cousin Shamsa Ford, wanasema samehe saba mara sabini, tafadhali msamehe mwenzio amekiri makosa, embu rudi kwa mumeo bana tafadhali, tafadhali rudi kwa mumeo"



# Q CHIEF

## HUTAKI KUONA MAKOSA YAKO?

MSANII wa Bongo Fleva, Q Chief, ameeleza hawezi kujutia kuhusu kauli yake kwa Mwana FA, kwani neno sawa na dawa.

Awali Q Chief ameonekana kwenye video fupi akimsema Mwana Fa kwamba ametafuta kiki na amefanya kitendo cha kitoto kwa kujitangaza kama amepata virusi vya ugonjwa wa Corona .

"Kila mtu na dunia nzima inamjua Q Chief, sio lazima ufe ndiyo watu wakusifu. Kauli yangu ni kama dawa, mimi sio mtu wa kushinda mitandaoni kila muda, video ile kutembea kiasi hicho inamaanisha bado nina umuhimu kwa watu na wanaamini kile ninachokisema".




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## INSTA-TWITTER



Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Muhimu** kuchukua tahadhari Corona inaua. Mwenyezi Mungu atuepushie-**Yusuph Mlela.**



**Wakati** huu ambao mpo likizo,vipepeo wetu tulieni nyumbani, hakikisha mnanawa mikono na kujilinda na Covid 19 ni virusi hatari sana,walinde na wale wote unaowapenda-**Rose Ndauka.**



**Miziki** sio kama nguo kila mtu avae, jiwe baada ya jiwe, piga kelele weweee-**Nandy.**

# Kuumbe!



# ANAPOTEA

## VANESSA MDEE ATAHADHARISHWA

BAADA ya mwimbaji nyota nchini, Vanessa Mdee, kuibuka na kusema sasa anajipa mapumziko ya muda, mashabiki wake wamemjia juu na kueleza anajiua kisanii.

Wiki hii, Vanessa amevunja ukimya kwa kuongelea ukimya wake na maamuzi yake ya kupumzika.

Akitumia video fupi kwenye ukurasa wake wa Instagram, mrembo huyo amesema kwa muda mrefu amefanya kazi ya muziki bila ya kupumzika, sasa ameamua kula maisha na mchumba wake ambaye ni mwigizaji, Rotimi, raia wa Nigeria.

Akizungumza kwa lugha ya kingereza, Vanessa, ameeleza kwa miaka 13 amefanya kazi bila ya mapumziko, jambo lililomfanya kujipa likizo ya muda.

***"Kwa miaka 13 nimefanya kazi bila mapumziko, hatimae nimepata muda kwa ajili yangu, kufanya ninavyovipenda na kuvitaka, nataka kuchukua muda kufurahia maisha, tuko hapa kwa ajili ya kuishi na kufurahia maisha" amesema Vanessa Mdee***

Wakati akiongea kwenye video hiyo, mara alijitokeza Rotimi, na kuongea kwa maneno ya Kiswahili "hatuachani"

Vanessa amewashukuru mashabiki zake kwa kumuunga mkono 'podcast' yake kwenye msimu wa kwanza na kuahidi kuileta sehemu ya pili kwa kujibu maswali mengi ya Mashabiki zake.

Baada ya kusambaa kwa kasi video hiyo, baadhi ya mashabiki wake wamemshauri kuwa makini kwani kuna hatari ya kupoteza kipaji chake.

"Tunavyomjua Vanessa ana tabia ya kupenda na kulewa mapenzi, asipokuwa makini anaweza kupoteza kipaji chake kwa ajili ya mwanaume," amesema Ashura Juma.

George Semkumbo, alimshauri msanii huyo kuweka usawa kati ya mapenzi na kazi yake na pale atakapolemea sehemu moja, matokeo yake yanakuwa mabaya na yanaweza kumshusha kisanaa.

Kabla ya kukutana na Rotimi, Vanessa, alikuwa na uhusiano wa kimapenzi kwa muda mrefu na mwanamuziki mwenzake, Juma Jux, ambaye waliachana mwishoni mwa mwaka jana.



# Filamu za Kihindi zilizowaliza Wabongo



**Na Adam Fungamwango**

KWA wale vijana wa miaka ya '80 na mwanzoni mwa '90, watakumbuka kumbi mbalimbali za sinema ambazo zilitamba nchini.

Kwa Dar es Salaam kulikuwa na kumbi kama Drive In Cinema, Odeon, Avalon, New Chox, Star Light, Empire, Empress, Cameo, na nyingine nyingi.

Wale watoto wa uswahilini kulikuwa na kumbi kama Milano na Morocco. Hata kwenye mikoa karibuni yote nchini Tanzania kulikuwa na kumbi kubwa ambazo zilikuwa zikionyesha filamu mbalimbali.

Vijana na hata watu wazima wa wakati huo alikuwa wapenzi wa filamu za Kihindi ambazo wakati huo hakukuwa na teknolojia na kutafsiri kama ilivyo sasa, lakini watu walizielewa vizuri na hata kuhadithia utadhani walikuwapo wakati filamu hizo zinachezwa.

Zipo filamu ambazo hadi leo hazifutiki kwenye kumbukumbu za watu wengi, japo kwa sasa ni watu wazima na wengine wameshakuwa wazee.

Zifuatazo ni filamu za Kihindi zilizoliza sana watu wakati huo.

### Andha Kanoon

Hii ndiyo filamu ambayo ililiza watu wengi kuliko yoyote ile ya Kihindi. Hadi leo kwa wale ambao hawajawahi kuitazama wanaweza kuangua vilio. Andha Kanoon ni filamu maarufu zaidi ya Kihindi hapa nchini wakati huo, ikichezwa na stelingi kipenzi cha wengi wakati huo, Amitah Bachchan.

Kisa kilichokuwa ndani ya filamu hiyo iliyotoka mwaka 1883, ndicho kilichosababisha wengi kulia. Ni hadithi ya askari mwaminifu kwa Serikali yake, lakini akafanyiwa zengwe na watu wabaya waliomo humo humo Serikalini pamoja na mhimili wa mahakama, kumsingizia ameua mtu kwa sababu tu ya kukataa kupokea rushwa wa wahujumu wa Serikali.

Miaka 30 ilipita akamaliza kifungo, lakini alipotoka alimkuta aliyeambiwa amemuua yuko jukwaani akiomba kura kwa wananchi ili awe mbunge, wakati Amitah akiwa amepoteza mke na mtoto alipokuwa gerezani.

### Hatya 'Yaya'

Nadhani filamu hii ya Kihindi itakuwa inafuatia, au inashika nafasi ya pili kwa kupendwa na watoto, vijana na watazamaji wengi wakati huo.

Inaitwa 'Hatya' ingawa Wabongo waliita 'Yaya' kutokana na dogo mmoja humo ndani ambaye alikuwa 'bubu', neno lolote alilotaka kuongea alitamka 'yaya'. Ilitoka mwaka 1988.

Stelingi kwenye picha hilo anaitwa Govinda. Inahusu misukosuko alioipata Govenda baada ya huruma yake ya kumuokota mtoto akaamua kumlea, lakini bila kumpeleka polisi.

Ulemavu wake wa kutoongea nao ukaleta tatizo. Ni mtoto aliyeokotwa baada ya wazazi wake kuuawa na yeye kukimbia. Wauaji walipotambua hilo, walitumia njia zote za kutaka kumuua yeye na Govinda ili kulinda siri, lakini pia walitumia baadhi ya polisi wasio waaminifu kuaminisha jamii kuwa Govinda ndiye muuaji.

### Adveture of Tarzan

Ni filamu moja kali ya Kihindi iliyotoka mwaka 1985, iliyopendwa na mashabiki wengi.

Ni kisa cha kijana wa aliyekulia msituni na kuwa kama nusu mtu, nusu mnyama, lakini akapendwa na binti mmoja wa tajiri aliyekwenda na familia yake porini kutazama wanyama mbugani.

Wanaompenda mrembo huo hawa vijana matajiri hawakumuacha salama, wakawa wanamuwinda kama mnyama ili wamuue, awaachie mrembo.

### Disco Dance

Filamu hii nayo ilileta matata sana nchini na duniani kote baada ya kutoka mwaka 1982. Stelingi alikuwa ni Mithun Chakraboty. Ina kisa na kijana mwenye kipaji cha muziki aliyetoka kijijini kwenda mjini kusaka maisha. Kipaji chake kikubwa, pamoja na kupendwa na wasichana warembo, kilisababisha kupata maadui wengi waliokuwa wakimuwekea mitego mara kwa mara ya kumuua.

### Ghatak

Ni filamu iliyotoka mwaka 1996 stelingi akiwa ni Sunny Deol. Jamaa anakwenda kijijini kumtazama baba na ndugu zake na kukuta watawala wametiwa mfukoni na tajiri mmoja ambaye anawafanya watu atakavyo hata kuwalaza mchana.

Pamoja na magumu anayopitia, lakini Deol anafanikiwa kuweka mambo sawa. Ni moja kati ya filamu hadi leo zinaweza kukutoa machozi.

# IMETOKEA

## Shimo jeusi angani linalomeza nyota

KUNDI la wanasayansi wa anga za juu nchini Marekani, wamegundua ushaidi wa kuwapo kwa shimo lenye rangi nyeusi angani.

Wanasayansi hao wanasema shimo hilo linatawanya wa kupasua vipandevipande nyota zinazolikaribia.

Shimo lenye ukubwa kama huo, ni vinavyokosekana kuonekana tangu ulimwengu ulivyouumbwa . Watafiti walitumia mionzi ya X-ray, pamoja na darubini ili kuona shimo hilo.

"Mashimo meusi yanayopatikana angani huwa hayaonekani kwa urahisi, hivyo basi ni muhimu kufikiria na kuamua maelezo mbadala kwa kila shimo", alisema Dkt. Daceng Lin kutoka chuo kikuu cha New Hampshire mjini Dutham Marekani, ambaye aliongoza utafiti huo.

Mwaka 2006, chombo cha Nasa kinachozunguka dunia kinachofahamika kama Chandra X-ray Observatory na XMM-Newton satelaiti ya Shirika la Ulaya ziliona picha ya nguvu ya X-ray iliyoitwa 3XMM J215022.4−055108.

"Hali ya picha hiyo ya X-ray ilikuwa inaweza kuelezewa kwa mazingira mawili kulingana na Dkt. Lin. Kuna uwezekano ipo mbali na nje ya galaxy ambapo shimo jeusi linameza nyota au ilitawanyika katika galaxy yetu", aliambia BBC News.

Ni eneo lenye nafasi angani ambapo hakuna chochote hata mwangaza kinaweza kuepuka.

Licha ya shimo hilo kutokuwa na jina, halipo tupu na badala yake lina idadi kubwa ya vitu vilivyojaa katika eneo dogo na hivyo kulipa nguvu kubwa ya mvuto wa kati au graviti.

Kuna eneo lenye mwanya katikati ya shimo jeusi kwa jina event horizon. Kitu kinachopita karibu na mwanya huo hakiwezi kuepuka mvuto wake na kinapoingia hakiwezi kupatikana tena.

Ili kutofautisha kati ya mazingira haya mawili, darubini ya Hubble Space ilielekezwa kwenye chanzo cha X-ray ili kubaini eneo lake sahihi.

Darubini ilitoa ushahidi kwamba X ray hiyo ilitoka sio tu katika chanzo kilichotengwa, bali katika mkusanyiko wa nyota nje ya galaxy.

Hili ndio eneo ambalo wataalam wa angani walitarajia kupata shimo jeusi la wastani. Mashimo makubwa meusi hupatikana katikati ya galaxy, kwa mfano, mwanga unaotoka angani unahifadhi shimo jeusi lililopo katikati kwa jina Sagittarius A*.

Lakini mashimo meusi ya katikati yamekuwa vigumu kuyapata kwasababu ni madogo na hayafanyi kazi vizuri ikilinganishwa na yale makubwa.

Aidha hayana vyanzo vya kufanya kazi kama mafuta na hayana nguvu zinazohitajika kuvuta nyota ndani ili kutoa mwangaza wa X ray.

Wataalam wa anga walilazimika kulipiga picha shimo moja jeusi lenye ukubwa wa wastani lilipokuwa likiimeza nyota. Dk Lin na wenzake walilazimika kupitia maelfu ya picha za XMM-Newton ili kuweza kuliona shimo hilo.

Mwangaza unaotolewa na mionzi ya X ray kutoka kwa nyota zilizopasuliwa vipande vipande, uliwaruhusu wanaanga kukadiria ukubwa wa shimo hilo kuwa mara 50,000 zaidi ya ukubwa wa jua.

Hili sio shimo jeusi la kwanza, lakini unapoona jinsi linavyopasua nyota vipande vipande linafanya ugunduzi huo kuwa na ushawishi mkubwa, kulingana na kundi la Dkt Lin.

"Ukichunguza kuhusu chanzo na ugunduzi wa mashimo hayo meusi, utapata majibu ya chimbuko la mashimo meusi makubwa ambayo hupatikana katikati ya galaxy", alisema Dk Natalie Webb kutoka chuo kikuu cha Toulose , Ufaransa.





## CHANGUDOA
## Shetani anaweza kuwa malaika?

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine binadamu anapitia kwenye mazingira magumu na tata, hadi abadilike na kuwa mtu mwema.

Kwa wale wanaokwenda kwenye makanisa, ni mashuhuda kwa watu wanaotoa ushuhuda kuwa alikuwa wachawi, majambazi, au wala rushwa, lakini baadaye wanatubu, wanamrudia Mungu na kuwa watu wema.

Hiki ndicho kisa kilichomo kwenye filamu hii itwayo 'Changudoa.'

Filamu hii imechezwa na wasanii kina Nassor Ndambwe, Flora Mvungi, Abdul Mhema na wengine wengi.

Inaanza kwa kumuonyesha kuwa Flora ni msichana ambaye kazi yake ni kuuza mwili.

Anafanya kazi ya ukahaba, ndiyo inayomfanya kupata mahitaji yake ya kila siku.

Filamu inamuonyesha kuwa yupo na mteja kwenye nyumba ya kulala wageni.

Lakini anafanya kitu cha ajabu, baada ya kuamka huku mwenzake akiwa amelala na kwenda kumkomba kila kitu na kutimka, wakati mteja wake akiwa kwenye usingizi fofofo.

Anapoamka hamkuti mwenzake kitandani na anashangaa kuona nguo zake zimetupwa chini na hatimaye kugundua kuwa amelizwa kila kitu na changudoa aliyemchukua.

Upande mwingine anaonekana Flora yuko na shoga yake wakishauriana ni jinsi gani ya kwenda kutafuta mabuzi wa kuwachuna.

Mara anakuja Abdul na kumuomba Flora wawe pamoja usiku huo. Wakiwa kwenye nyumba ya kulala wageni anavamia mtu mmoja anayejulikana kwa jina la Ndambwe ambaye anatoa bastola kumuonyesha Flora na kumwambia amlipe pesa zake, sivyo atammaliza. Hili linamuogopesha Abdul na kuamua kuchukua yeye jukumu la kulipa pesa hizo.

Abdul anaonekana kumpenda sana Flora kiasi cha kumuambia kuwa anahitaji kumuoa.

Kutokana na hilo, anaamua kumpeleka nyumbani kwake. Wanapofika wanakutaka na Ndambwe ambaye analianzisha vurugu.

Mwenye nyumba anatoka baada ya kuona nje kuna ugomvi, lakini anakutaka na mpangaji wake Abdul pamoja na Flora ambaye pia ameshawahi kumchukua na kwenda naye kufanya naye mapenzi gesti.

Sasa ugomvi unakuwa mkubwa zaidi kiasi cha Flora, kuwachoropoka na kutimua mbio kuepuka kupigwa.

Anapofika nyumbani anawapigia simu shoga zake kuwaeleza yaliyompata na jambo hilo lilimuathiri kisaikolojia kiasi cha kuamua kuchana na kazi hiyo.

Akaamua kufanya kazi ya kuuza maandazi, lakini kwa sababu hajaizoea, alijikuta sehemu kubwa ya maadazi akirudi nayo nyumbani na kuyatafuna yeye na shoga zake.

Alikaa na kufikiri, akili ikamtuma kurudia tena kazi yake ya uchangudoa. Huko tena alikutana na Abdul. Flora alitaka kukimbia akidhani atapigwa, lakini jamaa anamwambia hakuna na nia hiyo, ila azma yake iko pale pale ya kumuoa.

Flora alikataa kwa madai hana hadhi hiyo, lakini Abdul alimbembeleza na kumwambia kuwa kitu anachotakiwa kufanya ni kuanza ukurasa mpya akishakuwa mke wa mtu.

Flora alitafakari kazi ya uchagundoa na kuona tayari imeshamletea matatizo, huku kazi ya kuuza maandazi ikiwa hailipi, upande wa pili kuna mtu anamtaka awe mkewe, kitu ambacho ni nadra sana.

Mwishowe anakubali kuolewa na anaamua kubadilika kitabia. Abdul amuoa na kumuondoa sehemu ambayo amezoeleka na kwenda kuishi naye mbali na hapo. Akawa mke mwema.



# WALIA NA CORONA STAA MAREKANI ARUDISHA BIL 15

MWAKA 2020, umekuwa mchungu kwa wanandoa, Rande Gerber na Cindy Crawford, baada ya dili nono la kuuza nyumba kushindikana.

Wawili hao walikuwa wamepata ofa nzuri ya kuuza nyumba kwa bei ya juu, lakini kutokana na janga la vurisi vya corona, imewabidi kurudisha fedha baada ya wanunuzi kughairi.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Rande na Cindy, waliuza moja ya nyumba wanayomiliki huko Malibu, kwa dola milioni 6.5 sawa na shilingi zaidi ya bilioni 15 kwa familia moja inayoishi Ulaya.

Kiasi hicho kilikuwa kizuri kutokana na nyumba hiyo walikuwa hawaishi na ilikuwa ikihudumiwa na watu kwa malipo.

Kutokana na janga la corona, Marekani imepiga marufuku usafiri kutoka nchi za Ulaya na kusababisha wanunuzi hao kushindwa kwenda kukabidhiwa nyumba yao, lakini walikuwa wamelipa pesa hizo kwa njia ya mtandao.

Familia hiyo iliwaomba Rande na Cindy kuwarudishia pesa zao kwa sababu wao haitakuwa rahisi kwenda Marekani kutokana na zuio hilo.

Hata hivyo, Rande analalamika suala hilo kwamba limemkosesha pesa kutokana na kuvunjwa kwa mkataba wao.

"Wakati mtu anaweza kufuta mkataba kwa sababu ya virusi vya corona? Tunaweza kufikiria mara mbili kutokana na majanga haya ya asili," amesema Rande.

Katika mikataba ya mauziano kuna vifungu ambavyo vinamlinda mnunuzi endapo kutatokea majanga yasiyotabirika kama ghasia, vita, migomo na mapambano ya magonjwa hatari.

Kuna biashara kadhaa ambazo haziruhusu watu kutumia vifungu vya nguvu kutoka nje ya mikataba.

Staa kutoka Ufaransa, Thomas Keller, anaishitaki kampuni ya bima akitaka apewe tamko na jaji kulipwa bima baada ya kupata hasara katika biashara zake.

Haya hivyo kampuni zingine za bima zimepinga, zikisema serikali nyingi zimepiga marufuku watu kutoka nje kwa kuhofia kusambaa kwa virusi vya corona, hivyo wao hawawajibiki kwa lolote katika kipindi hiki.

# Davido amkubali Wizkid



MWANAMUZIKI maarufu wa Nigeria, Davido, amerudia kumwagia sifa msanii mwenzake Wizkid, akisema kibao chake cha 'Wiz Party' ni moto mwingine ulioshtua dunia.

Wizkid na Davido wamebaki katika chati ya Billboard na kuwaletea mauzo mazuri.

Akiandika kwenye ukurasa wake wa Instagram mubashara, Davido alisema

"Pia narudi kutoka Atlanta, US watu wanasema huyu ni kijana wasichana wanampenda...Unajua huyu ninayemzungumzia ni Wizkid," amesema davido.



## Burna Boy usiwe mkali, jibu hoja

MUDA mrefu watu wanamzungumza staa wa muziki wa Nigeria, Burna Boy, kwamba nyimbo zake zinafanana na zile za mwanamuziki wa zamani Fela Anikulapo Kuti.

Burna Boy alichukua muda wake kujibu maswali ya mashabiki wake na swali aliloulizwa kuhusu kufanana nyimbo zake na Fela zilimfanya kukasirika na kujibu ovyo.

"Ni upuuzi kusema haya, msilinganishe nyimbo zangu na zile za Fela, Fela alikwenda mbali na kile unachofikiri wewe," amesema.

## Funke tumeikubali 'Omo Gheto' inatesa

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Funke Akindele, ametambulisha kazi yake mpya inayoitwa 'Omo Ghetto'.

Funke alianza kutambulisha ujio wa filamu hiyo mwezi Februari kwa kuweka picha zake na msanii mwenzake Eniola Badmus katika ukurasa wa Instagram.

Baadhi ya vipande vya filamu 'Omo Ghetto the Saga' vilichukuliwa katika mji wa Dubai.





## Duh! Aaron umepigwaje na demu wako?

POLISI nchini Marekani, wamemkamata mchumba wa msanii Aaron Carter, kwa kosa la kumchapa mwimbaji huyo.

Melanie Martin alikamatwa baada ya Carter kupiga simu polisi akilalamika kupigwa na mchumba wake huyo wakati wakiwa nyumbani.

"Huwezi kusubiri mtu mmoja anayekulea vibaya, ukibaini anakudhalilisha kwa jambo lolote tafuta ya baadae," aliandika Carter baada ya tukio hilo.

## Umeme wamkera Mercy kuzuizini

STAA wa filamu kutoka Nigeria, Mercy Aigbe, ameibua mjadala mtandaoni baada ya kukasirishwa na kitendo cha umeme kukatita wakati wapo kwenye kuzuizi cha nyumbani.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Mercy amesema wamechanganyikiwa kwa kukosa umeme wakati wapo ndani kutokana kusambaa kwa virusi vya COVID-19.

Serikali ya nchi hiyo imewaagiza wananchi wake kubaki majumbani kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huo ambao tayari umesababisha vifo vya watu wawili.



MAKALA



KALAMU YA MWALIMU

# Wanafunzi tumieni likizo ya Corona kujisomea

Na Reubeni Lumbagala

UGONJWA wa Corona ambao unasababishwa na virusi vya COVID 19, umekuwa janga kubwa katika mataifa mengi ikiwamo Tanzania.

Kutokana na kuwa hatari kwa maisha ya watu, serikali imechukua hatua ya kuzifunga shule zote za awali, msingi, sekondari, vyuo vya kati na vile vikuu kwa muda wa mwezi mmoja.

Tamko hilo lilitolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Machi 17, mwaka huu lilikuwa na lengo la kuepusha virusi hivyo kutosambaa ndani ya jamii na kusababisha athari kubwa.

Pia serikali imepiga marufuku mikusanyiko ya watu wengi katika Nyanja ya siasa, michezo, makongamano, semina na sherehe mbalimbali. Kutokana na tamko la serikali, wanafunzi wote nchini wamerejea majumbani kwao. Hoja ya mjadala wa leo ni kuwakumbusha wanafunzi wajibu wao wa kujisomea kwa bidii katika kipindi hicho.

Muda wa mwezi mmoja uliotolewa na serikali wa kunusuru hatari ya kusambaa kwa ugonjwa huu, kwa wanafunzi makini ni fursa nzuri ya kujisomea kwa bidii.

Mapumziko haya si muda wa kusafiri kutembelea ndugu, jamaa na marafiki kama baadhi wanavyofikiri. Mapumziko haya pia si muda wa kuzurura mitaani bila kuwa na mambo ya msingi ya kufanya.

Vilevile, si muda wa kushinda sebuleni kuangalia sinema. Ni muda mzuri kwa wanafunzi kujisomea na kujikumbusha yale aliyojifunza shuleni kabla ya kufunga shule.

Kabla ya kufungwa shule , wanafunzi wanaosoma shule za msingi na sekondari hadi kidato cha nne walikuwa wakijiandaa kufanya mitihani ya robo muhula. Kwa wanafunzi wa kidato cha sita walikuwa wakijiandaa kufanya mtihani wa Taifa kwa kumaliza masomo yao mwei Mei.

Halikadhalika, kwa wanafunzi wa vyuo vya ualimu, nao walikuwa wakijiandaa kumaliza mitihani yao ya kuhitimu astashahada na stashahada zao mwezi Mei mwaka huu. Hivyo, likizo hii imekuja kipindi ambacho taasisi mbalimbali za elimu zilikuwa katika harakati za kufanya mitihani mbalimbali ambayo ni muhimu kwa mustakabali wa wahitimu.. Kwa mantiki hii, ugonjwa wa Corona umeathiri kwa kiasi kikubwa ratiba na mihula ya elimu nchini.

Niwakumbushe wanafunzi kuwa mitihani hiyo ipo na inawasubiri siku watakaporejea shule waweze kuifanya. Wanafunzi wasidhani kufungwakwa shule ni salama yao ya kutofanya mitihani na hivyo kuzembea. Wanafunzi wote nchini wana wajibu wa kutumia vizuri muda wa mwezi mmoja kujisomea ili kujiongezea uelewa wa masuala mbalimbali aliyojifunza shuleni.

Pamoja na umuhimu wa kujisomea katika muda huu wapumziko, wachukue tahadhari zote ili kujiepusha na hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa Corona. Ni vyema wanafunzi wakafuatilia kwa karibu vyombo vya habari ili kupata elimu ya ugonjwa wa Corona.

Wanafunzi watulie majumbani, waepuke mikusanyiko isiyo ya lazima, wanawe mikono kwa maji safi yanayotiririka, waepuke kusalimiana kwa kupeana mikono, kukaa mbali na mtu mwenye dalili za mafua na mwenye historia ya kusafiri katika nchi zenye mlipuko wa ugonjwa huu nk.

Tahadhari hizi zikichukuliwa kwa umakini mkubwa, wanafunzi watakuwa salama dhidi ya maambukizi ya Corona. Pamoja na umuhimu wa wanafunzi kujisomea na kujikinga na ugonjwa wa Corona kwa wakati huu wa mapumziko, wanatakiwa kuwa raia wema na wenye nidhamu kwa familia zao na kwa jamii.

Uwepo wao uwe chachu ya kusaidia kazi ndogo ndogo kama kuosha vyombo, kupika, kufua nguo za wazazi wao, kulisha mifugo, kulima bustani za mboga nk.

Kwa ujumla, mapumziko haya yaliyosababishwa na uwepo wa ugonjwa wa Corona nchini, yana nafasi kubwa ya kuendelea kumpa mwanafunzi muda wa kutosha wa kujisomea.

Pamoja na jukumu kubwa walilonalo walimu la kufundisha wanafunzi, muhimu kama mtajikumbusha yale waliyofundishwa na walimu wao pamoja na kujisomea vitabu kwa ajili ya kupata maarifa.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**

**Moani: (+255) 764 666349**

# Safari zisizo na ulazima ziokoe fedha za umma

Na Gaudensia Mngumi

KATIKA kampeni za kupambana na corona ndiyo wakati wa serikali 'kusevu pesa' ili ziingizwe mikononi mwa wananchi kutokana na kupunguza safari zisizo za lazima zikiwamo za ndani ya nchi.

Mapema 2016, awamu ya tano ilipoingia madarakani ilibainisha kuwa eneo moja ambalo fedha za Watanzania zililiwa bila huruma na kutangaza kulipiga marufuku lilikuwa ni safari za ughaibuni ambazo viongozi na watendaji wengi walizitumia kwa manufaa binafsi.


Kufikiwa kwa hatua hiyo ni kama maombi ya Watanzania wengi yalisikika kwani wakati hakukuwa na dawa hospitalini viongozi na watendaji wengi walidaiwa kupishana angani kwa safari za ughaibuni hawa walikuwa ni pamoja na mawaziri, wabunge na maofisa wa ngazi mbalimbali serikalini.

Zama za safari za ughaibuni, ziara za viongozi zilikuwa hazikauki wakiwamo za manispaa au halmashauri za wilaya kuanzia madiwani, wenyeviti wa halmashauri na wakurugenzi ambao walisafiri kwa maelezo kuwa wanafanya ziara za mafunzo ambazo mbali na kujikusanyia posho za kujikimu hakuna tija inayaoonekana kwa halmashauri zao.

Ndiyo maana uamuzi ya Rais John Magufuli, alipoanza kuongoza serikali alianza na kuzipunguza na hata kuzifuta kwa lengo la kutumia rasilimali za nchi kwa manufaa ya wote siyo kunemeesha wachache, kupitia dirisha la safari za ughaibuni.

Pengine na huu ujio wa corona unaelekeza watu kupunguza safari zisizo za lazima si raia peke yao hata viongozi nao agizo hilo linawahusu , ndiyo maana kwenye kupeana tahadhari suala la kusafiri bila sababu za msingi linapewa kipaumbele pia, kwani pamoja na kuokoa fedha za serikali zilipo wahusika wanajiepusha na kuambukizwa au kusambaza corona.

Kwa hiyo kutokana na kusambaa kwa corona mathalani kuna viongozi wanaotakiwa kufungua mikutano, semina au kuzindua kazi mbalimbali mikoani katika maeneo mbalimbali yanayohitaji kusafiri, nao waone kuwa si lazima wafanye hizo kazi wawaachie wengine kufanya hivyo, kwani vitu hivyo vimepigwa marufuku.



**TEKNOLOJIA**

Hata bila ya corona huu pia ni wakati wa kutumia teknolojia. Ni wazi kuwa zama hizi za teknolojia kuimarika iwape funzo viongozi kwani huenda hawana sababu za kujipangia safari nyingi za kuzunguka mikoani. Waanze kufikiria matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehema) inayopunguza ziara hizo

Utaalamu wa 'tele conference' ambayo ni mikutano ya mitandaoni, ndiyo iliyofanyika hivi karibuni tena ikihusisha wajumbe wa kanda wanachama wa Ushirikiano wa Kusini mwa Afrika (Sadc) . Inaweza kutumiwa kukutanisha watendaji wa halmashauri na mikoa mbalimbali kujadili masuala na kufanya muamuzi bila kusafiri na kutumia gharama lakini pia kusambaza corona.

Kuna mawasiliano ya mitandao yanayotumia mifumo ya kijiografia iitwayo GPS au Google Earth ambayo ni kama kitabu cha ramani (Atlas) inayoweza kuonyesha kila kitu kwenye uso wa dunia ikiwamo maeneo viongozi wanayokusudia kuyatembelea.

Wataalamu na viongozi wa serikali wanaweza kutumia GPS kuangalia miradi inayojengwa vijijini iwe zahanati, shule, barabara na madaraja hata bila kusafiri. Pengine ziara zinaweza kufanyika kutizama kiwango cha ubora na si vinginevyo na si lazima kiongozi aende anaweza kutumia wataalamu kuhakiki.

Kwa hiyo pamoja na kuenea kwa corona ni vyema pia teknolojia itumike kupunguza matumizi ya fedha za umma hasa ikizingatiwa kuwa mkongo wa taifa unapita katika kila halmashauri.

Aidha, kwa kutumia GPS inawezekana kuona na kuutambua ukweli kuwa kazi zinazofanyika zimefikia kiwango gani na pia kutumia teknolojia hiyo kuhakiki ubora wa kazi hasa majengo.

MAKALA

# Kipande cha kilomita tano kilivyowatoa jasho wasafiri

**Na Epson Luhwago**



Abiria wakitembea kwa shida baada ya gari kukwama. **PICHA ZOTE: EPSON LUHWAGO**

HAKUNA tofauti kati ya mwaka 2008 na mwaka huu. Hivyo ndivyo inavyoweza kuelezewa kutokana na ubovu wa kipande cha barabara yenye urefu wa kilomita tano.

Kipande hicho ni cha Kisiwa hadi Mto Lukosi, maarufu kama Njia Panda ya Idete na Kiwalamo, katika wilaya ya Kilolo mkoano Iringa.

Tofauti kati ya miaka 12 na mwaka huu hakuna kwa sababu adha wanazopata watumiaji wa njia hiyo iko palepale. Kipindi cha masika huwa shida kubwa kutokana na tope na utelezi. Sababu kubwa ni udongo wa eneo hilo kuwa wa mfinyanzi na sehemu zingine tifutifu.

Kama ilivyokuwa adha iliyotokea hivi karibuni na inayoendelea, ndivyo ilivyotokea Februari 17, 2008 wakati msafara wa msiba wa Mzee Raphael Luhwago ulipokwama eneo hilo kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Hali hiyo iliwalazimu watu waliokuwa kwenye basi dogo aina ya Toyota Coaster kuanza kulisukuma bila mafanikio. Hivyo ndivyo ilivyo hata sasa kwani ni taabu kubwa kwa magari kupita eneo hilo.

Kutokana na ubovu huo, kipindi kama hiki ambacho mvua inanyesha kwa kiwango cha juu, kuanzia wakati wa vuli, ni magari machache yanayoweza kupita. Magari yale yaliyozoea lami au kokoto yakipita hapo yanaweza kukaa mpaka mvua iishe. Hali hiyo ilishuhudiwa kwa mara nyingine hivi karibuni wakati baadhi ya wananchi wa kijiji cha Kiwalamo na vijiji jirani, waishio maeneo mbalimbali walipokwenda kijijini hapo kwa ajili ya mazishi ya mpendwa wao, Tufuwage Gilla, aliyefariki dunia jijini Dar es Salam.

Wananchi hao walioungana na wenzao Iringa kwenda kwenye mazishi hayo, walisafiri salama kutoka Dar es Salaam kwa basi maalum lakini walipofika Kidabaga Machi 20, mwaka huu saa 12:00 alfajiri, walipata habari ambazo ziliwakatisha tamaa kwamba wanapaswa kuishia hapo kwa kuwa hali ya barabara mbele ya safari si nzuri kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Taarifa hiyo iliwafanya ndugu hao kuanza kufikiria usafiri mbadala wa kusafirisha abiria pamoja na mwili wa marehemu. Njia pekee ilikuwa kukodi gari la Shule ya Sekondari ya Lutangilo-Land Rover 110 Defender, ambalo lilielezwa kuwa ndilo pekee lenye uwezo.

Mbali na gari hilo, yalifanywa mawasiliano na Diwani wa Idete, Bruno Kauku, ambaye pia gari lake aina ya Toyota Land Cruiser Pick-up limekuwa likibeba abiria wakati wa masika kutokana na mabasi yanayofanya safari kati ya Iringa na Idete kushindwa kufika huko.

Mawasiliano yalifanywa na kuwapata wahusika wote. Kwa bahati nzuri, gari la Lutangilo lilikuwa Kidabaga huku lile la Diwani likiwa Idete na lilifika wakati muafaka.

**HOFU YAINGIA**

Wasafiri hao wakiwa na matumaini ya kufaulisha mwili pamoja na wao kusafiri kwenda Kiwalamo, walikumbwa na hofu baada ya kuambiwa gari la Lutangilo limepata hitilafu katika usukani huku gari la Diwani lilidaiwa haliwezi kupita eneo korofi.

Baada ya taarifa hizo, wazo jipya lilipatikana kwamba basi lililotoka Dar es Salaam linaweza kufika kijiji cha Ikelamwa na mpango ukafanyika kutekeleza hilo huku jitihada za kutengeneza gari la Lutangilo likiendelea.

Hatimaye gari tegemeo la Lutangilo lilikamilika majira ya saa 3:30 asubuhi na kwenda Ikelamwa kuungana na wasafiri wengine wa basi la msiba. Muda mfupi wasafiri wote waliungana na kuamua kupanda gari dogo la Lutangilo kwa awamu kufika Kiwalamo, jambo ambalo wote walifika msibani saa 8:30 alasiri.

Baada ya kuwasili kijijini, baadhi ya waombolezaji walionyesha furaha huku wakimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwafikisha salama. Hata hivyo, walionyesha masikitiko yao kutokana na kipande hicho kutokutengenezwa na kuwafanya wananchi kupata shida kila mvua inaponyesha.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Hoffman Kisiya, alisema tatizo la kipande hicho ni sugu kwa kuwa limekuwa likizungumziwa katika vikao mbalimbali. Pia alibainisha kuwa hata Halmashauri ya Wilaya na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wanaifahamu adha hiyo kwa sababu wamekuwa wakielezwa mara kwa mara.

"Kinachosikitisha ni kwamba barabara hii iko katika shamba la kampuni ya New Forest inayomiliki shamba kubwa la miti katika eneo hili na haijachukulia uzito wowote kuirekebisha. Lakini bado tuna matumaini kwamba ipo siku utapatikana ufumbuzi," alisema Kisiya.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kilolo, Killian Myenzi, ambaye ni mzaliwa wa Kiwalamo na mmoja wa wasafiri kwenye msiba huo, alisema ana matumaini ya kupatiwa ufumbuzi wa eneo hilo kwa sababu Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) imeliweka katika mpango.

"Lakini pia kuna taarifa kuwa New Forest mwakani wataanza kuvuna miti kwa ajili ya nguzo za umeme, hivyo watatumia magari makubwa kusafirisha bidhaa hiyo. Kwa vyovyote vile ni lazima watengeneze barabara hiyo hasa kipande kile korofi. Unadhani watasafirisha nguzo kwa barabara hii ilivyo? Lazima watengeneza ili magari yao yapitishe nguzo," alisema.

Meneja wa Tarura Wilaya ya Kilolo, Mhandisi Silvanus Ngonyani, alipoulizwa hatima ya kipande hicho alisema ofisi yake inatambua changamoto ya kipande hicho cha barabara na kuahidi kuipatia ufumbuzi.

"Kipande cha Kisiwa hadi Kiwalamo kipo kwenye mpango wa kukifanyia kazi kwa kutengeneza maeneo yote korofi. Kwa ujumla barabara nyingi za Kilolo hasa vijijini zimeharibika kwa sababu ya mvua zinazoendelea kunyesha. Baada ya kumalizika kwa masika tutaingia kazini," alisema Ngonyani.



Dereva akiangalia namna ya kukwamua gari.

MAKALA

## KUJIKINGA NA COVID 19

# Nani anatakiwa kuvaa barakoa?

Na Mwandishi Wetu



IDADI wagonjwa wa virusi vya Covid-19, Afrika Mashariki inaongezeka baada ya Kenya kufikia 110 baada ya watu wengine 29 kuthibitishwa.

Waziri wa Afya wa Kenya, Mutahi Kagwe amesema kwamba watu wengine wawili wamepoteza maisha kutokana na maambukizi ya virusi hivyo.

Amesema kwamba idadi hiyo inaongeza idadi ya watu waliofariki kutokana na ugonjwa huo kufikia watatu.

Katika ukanda wa Afrika Mashariki, Rwanda inaongoza kwa kuwa na wagonjwa 85, Uganda 45, Tanzania 20 na Burundi mgonjwa mmoja.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Marekani ndio Taifa linaloongoza kwa kuwa na wagonjwa 245,116, ikifuatia Italia 15,242 na Ujerumani inashika nafasi ya tatu kwa wagonjwa 84,794.

China ambayo imekuwa chimbuko la ugonjwa wa corona kwa sasa imetangaza ukuudhibiti ikiwa na wagonjwa 82, 464.

Hata hivyo, kumeena mjadala mkali baada ya wataalamu wa China kuwalaumu wenzao wa Ulaya kushindwa kuwelimisha watu kuvaa barakoa kama njia ya kudhibiti maambukizi.

Kutokana na mjadala huo, WHO imesema inaangalia kwa makini suala hilo, inafikiria namna ya kuwashauri watu wote kuvaa kifaa hicho kama njia ya kuepuka kupata virusi vya corona.

Lakini imeonya kama kifaa hicho hakitatumika ipasavyo, inaweza kuongeza kiwango cha ugonjwa huo kwa watu wasiokuwa na elimu sahihi ya kutumia.

Inasema kwa wakati huu ni aina mbili tu za watu wanafaa kuvaa barakoa.

Barakoa za upasuaji hazijapendekezwa kwa matumizi ya umma kwa sababu iinaweza kuchafuliwa na kukohoa, kupiga chafya au unapoivaa na kuivua.

Virusi vya corona vinasambazwa kwa matone mate au makamasi ambayo yanaweza kusambaa hewani, pale wale walioambukizwa wakiongea, wakikohoa au kupiga chafya.

Virusi vinaweza kuingia mwilini kupitia macho na mdomo baada ya kugusa vitu vilivyopata maambukizi. ES

Haishauriwi kutumia barakoa iliyotengenezwa nyumbani kwa sababu hakuna uhakika kuwa itatoa kinga ya kutosha au la.

Hata kama barakoa za aina hiyo zikitumika kwa usahihi, lakini kitambaa hakijathibitishwa kuwa na ubora wa kukinga, hivyo ni inaweza kuwa hatari.

Mara nyingi kitambaa hicho kinatumika zaidi ya mara moja.

Katika hospitali mbalimbali, barakoa za aina tofauti zinatoa ulinzi wa viwango tofauti.

Barakoa aina ya FFP3, N95 na FFP2 ni bora zaidi kutokana na kufanya kazi ya kuchuja hewa wakati mtu anapovuta

Wataalam hawashauri watu wa kawaida, barakoa hizi ni kwa ajili ya wahudumu wa afya ambao wapo karibu zaidi na wagonjwa wa corona na wapo katika hatari kubwa ya kupata majimaji kutoka kwa waathirika.

**GLOVU INATUMIKAJE?**

Glovu pamoja na mavazi mengine ya kujilinda yanashauriwa kutumiwa na wahudumu wa afya walio kwenye maeneo hatarishi.

Wafanyakazi walio katika hatari kubwa zaidi wanashauriwa kuvaa barakoa zenye ulinzi mkubwa zaidi na sio za vitambaa vya kawaida, glovu na miwani ya kujikinga.

Watu wa kawaida hawashauriwi kutumia glovu au vifaa zaidi vya kujikinga

Kujilinda dhidi ya virusi vya Corona unashauriwa yafuatayo

Nawa mikono kwa maji na sabuni mara kwa mara, angalau kwa sekunde 20 baada ya kurudi nyumbani

Tumia dawa aiana ya 'sanitizer' kama hakuna maji na sabuni

Ziba mdomo wako kwa tishu au kitambaa na sio mikono yako ukiwa unapiga chafya ,weka tishu uliotumia katika pipa la taka na unawe mikono yako

Usishike macho,pua au mdomo kama mikono yako michafu.



# MAAFA RUFIJI

## ■1974 jeshi lilitumika kunusuru walionasa
## ■2020 yamemeza vijiji, barabara, madaraja

**Na Moshi Lusonzo**

MWAKA 1974, Wakazi wa Wilaya ya Rufiji, walishuhudia kwa mara kwanza mafuriko makubwa yaliyosababisha vifo, mifugo na mazao yao kuteketea kwa maji.

Mto Rufiji unashika nafasi ya kwanza kwa ukubwa nchini, Mto huu unaunda ukanda mpana wa bonde lenye rutuba hapa nchini.

Katika zama hizo kabla ya ujenzi wa daraja linalovuka kufika ng'ambo ya pili, ilikuwa sharti kutumia ama pantoni au mbadala wa mtumbwi na zaidi ya hapo ni kuogelea, mtindo ambao ukiamua ujue unaweka roho mkononi.



Ingawa inabeba jina la mto, lakini thubutu kuuvuka upana na mitikisiko ya maji ndio utakuonyesha ni zaidi ya mto. Kwa kifupi, 'imeshatafuna' roho za wengi na uharibufu usiohesabika mashamba, kwa makazi.

Kwa wale ambao umri wao 'umekuchwa' watakumbuka karibu katika kila msimu wa mvua, Radio Tanzania maarufu RTD hakukosekana simulizi za athari zake. Wakazi wa Kusini mwa nchi, wana mengi zaidi ya hayo.

Kuepuka maafa hayo katika maeneo jirani kila kukicha, ndio ilizaa vijiji vingi vilivyo mbali na bonde la mto huo, ambako ni maarufu kwa kilimo cha mpunga hadi kesho.

Hapo nitadodosa baadhi ya vijiji kama Ikwiriri, Muhoro, Mkongo, Kilimani, Kipo, Mtanza, Mloka na Msona vilianzishwa kwa lengo la kuwanusuru watu na mafuriko.

Hilo halikuja hivi hivi! Ni uamuzi mgumu wa hayati Mwalimu Julius Nyerere, katika kutafutia ufumbuzi wa kudumu raia wake waliolipenda sana bonde hilo kwa ajili ya kufuatilia kilimo cha mpunga, baada ya kutokea maafa makubwa takribani miongo mine na nusu iliyopita.

Mwaka 1974, Rais Nyerere, alituma vikosi vya jeshi vikapige kambi katika bonde hilo, kuwaokoa watu waliokwama kwenye mapaa ya makazi yao yaliyozingirwa na maji

Kimsingi, mto huu unatokana na kuungana kwa mito mingine mikubwa ya Ruaha, km 85,554, Kilombero, km 40,330 na Luwegu wenye km 25,288.

Kilomita zingine 32,619 ndizo unaunda mto Rufiji ambao unaishia bahari ya Hindi, Eneo hili ndilo lenye maafa kila miaka kutokana na kukusanya maji mengi.

Mto Rufiji umepita katikati ya bonde lenye upana wa km 183,791, sawa na asilimia 20 ya nchi ya Tanzania.

Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa bonde la mto Rufiji katika uzalishaji mali, watu na serikali wamekuwa wakiwindana kama paka na panya.

Wakati serikali inashauri watu kuacha kuishi maeneo hayo na badala yake wawe wanalima pekee, lakini wakazi wa maeneo hayo wanaona kama wanapigiwa gita lisilo na sauti tamu, wao wanaendelea kulima na kujenga nyumba za kudumu za kuishi.

Hata hivyo, mafuriko mengine yalitokea mwaka mwaka 2016, lakini haya hayakuwashtua kwani hayakuwa na madhara makubwa.

Mwaka huu wakazi wa wilaya hiyo, wameshuhudia mafuriko mengine, lakini safari hii yamekuwa mabaya kupita yale ya mwaka 1974. Safari hii kaya zaidi ya 300 zenye watu wakazi 50,000 wamekosa makazi baada ya nyumba zao kuzama.

Katika kile kinachoelezwa mafuriko yalikuwa makubwa zaidi ni pale hata vijiji ambavyo kihistoria havikupata athari hizo, vimezingirwa na maji na kusababisha wakazi wake kukimbia na wengine kuokolewa.

**BUNGE LATAKA TAARIFA YA SERIKALI**

Juzi Bunge liliingilia kati kwa kuilekeza Serikali kuja na taarifa rasmi kuhusu ukubwa wa maafa yaliyotokea na kusababisha maelfu ya wananchi kukosa makazi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Spika wa Bunge, Job Ndugai, wakati akijibu hoja ya Mbunge wa Rufiji, Mohammed Mchengerwa (CCM).

Mbunge huyo katika hoja yake alitaka kujua Serikali inachukua hatua gani kuwasaidia wananchi wa Rufiji, ambao wamekumbwa na maafa na kusababisha wakose makazi ya kuishi na kubaki wakihangaika.

"Mheshimiwa Spika, Rufiji kumekuwa na maafa makubwa yaliyosababishwa na mvua kuliko maeneo mengine yote nchini, mpaka sasa wananchi takribani 20,000 hadi 50,000 hawana makazi ya kuishi,"

Akaendelea "Hawana chakula na wanahangaika sana kuokoa maisha yao, je, kama Bunge tunachukua hatua gani ili kuwaangalia hata hawa wananchi wanyonge ambao wako kwenye maafa ya mafuriko," akahoji Mchengerwa.

Spika Ndugai, pamoja na kutoa pole kwa mbunge na wakazi wa Rufiji na wa Kibiti, akasema mafuriko ya aina hiyo yaliyotokea katika eneo hilo, hayajapata kutokea na ni makubwa sana na kwamba anaamini Serikali imesikia ujumbe wa mbunge huyo.

"Tunapokea ushauri wake mheshimiwa mbunge, Mheshimiwa Jenister (Mhagama) ambaye ndiye Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, masuala ya maafa yako chini yake, wakati utakapofika atatupa taarifa kama Bunge," akasema Ndugai.

**HAKUNA KILICHOBAKI**

Mafuriko hayo yanaelezwa kuwa mabaya zaidi kiasi cha kukata mawasiliano ya ndani ya Wilaya ya Rufiji na kuziacha zaidi ya kaya 350 bila makazi.

Mafuriko hayo yameharibu miundombinu ya barabara, ikiwamo inayotoka Kibiti kwenda katika eneo la mradi wa umeme katika maporomoko ya Mto Rufiji ambako magari yenye vifaa yalikwama ndani ya maji.

Pia, baadhi ya barabara zinazounganisha kata 13 za Rufiji hazipitiki kutokana na makaravati kusombwa na maji,

Mkazi mmoja wa Muhorio, Ally Ngamba, anasema hali katika eneo hilo ni ya kusikitisha kutokana na watu wengi kukosa chakula, mavazi na sehemu ya kujihifadhi.

Anasema pamoja na serikali na watu binafsi kusaidia, lakini mahitaji yamekuwa makubwa kiasi ambacho kinaweza kuleta tatizo lingine la kijamii.

"Watu wanalala nje kwa wale waliokosa ndugu wa kuwahifadhi, hawana vyakula wala nguo za kuwahifadhi kwani kila kitu vimeteketea kwa maji," anasema Ngamba.

Asha Mzuzuri, anasema hakuna mali waliyookoa wakati mafuriko hayo. Mifugo yao na mazao yamekwenda na maji jambo ambalo limewarudisha nyuma.

"Tulikuwa na ng'ombe watano na shamba la mpunga, vyote vimekwenda na maji hatuna kitu sasa hivi," Asha anasema huku akitoa machozi.

**BARABARA, ZAHANATI, SHULE ZAATHIRIKA**

Miundombinu ya barabara, shule na zahanati kuathirika na mafuriko katika kata 13 za wilaya hiyo.

Muhoro na Chumbi ni miongoni mwa kata zilizoathirika sana na maafa hayo, ambapo kwa sasa madaraja matatu yaliyopo barabara ya Nyamwage - Utete inayoelekea makao makuu ya wilaya hiyo, Utete imeharibika kiasi ambacho haipitiki tena.

Daraja lililopo kwenye barabara ya kuelekea Mradi wa kufua umeme wa Mwalimu Nyerere, nalo limeathirika.

Daraja la Mkapa linaloanzia Ikwiriri hadi kijiji cha Nyamwage, limeonyesha dalili za kubomoka, hali inayotishia kukatika kwa mawasiliano na mikoa ya kusini.

**SERIKALI YATOA KAULI**

Akizungumza baada ya kukagua athari za maafa hayo, Mkurugenzi Idara ya Uratibu wa shughuli za Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kanali Jimmy Matamwe, alielekeza kamati za usimamizi wa kuanzia ngazi ya kijiji hadi wilaya, ziwajibike kutekeleza operesheni za dharura.

"Nimezishauri kamati za usimamizi wa maafa katika wilaya hii kuwa na mipango ya muda mfupi ya kuhakikisha barabara zinapitika kipindi chote ili wananchi wasishindwe kutumia miundombinu hiyo," anasema.

"Zipo barabara zinaunganisha mikoa ya kusini na zipo barabara zinawasaidia wananchi kuweza kufikia huduma za kijamii,"anasisitiza Kanali Matamwe.

Mkuu wa wa wilaya hiyo, Juma Njwayo, anasema misaada wanayoendelea kupokea kutoka kwa watu na taasisi binafsi na serikali itakuwa ni msaada mkubwa.

"Tunaishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutuletea magodoro, mikeka, vyandarua, ndoo na sabuni na naamini kamati za maafa zitawajibika kugawa vifaa hivi kwa mujibu wa taratibu za menejimenti ya maafa, " anasema Njwayo.



HABARI KIMATAIFA

# Wagonjwa corona wafika milioni moja

**LONDON, Uingereza**

ZAIDI ya watu milioni moja wamethibitishwa kuathirika na virusi vya corona, kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Chuo cha Johns Hopkins.

Karibu watu 53,000 wamepoteza maisha na watu 210,000 wamepona kwa mujibu wa ripoti za chuo hicho.

Marekani ina wagonjwa wengi zaidi, huku watu waliopoteza maisha wanafikia 1,000.

Ugonjwa huu wa Covid-19, ulianzia China miezi mitatu iliyopita na kusambaa kwa kasi duaniani.

Ingawa ripoti hiyo inaeleza kuthibitishwa idadi hiyo, inakisiwa watu wengi zaidi wameathirika na virusi vya corona.

Katika usaambaaji wa ugonjwa huo kwa kipindi cha mwezi mmoja na nusu, watu 100,000 wamethibitika kuambukizwa. Watu milioni moja ilifikiwa wiki iliyopita baada ya maambukizi kuwa zaidi ya mara mbili.

Karibu robo ya watu walioathirika na virusi, wamerekodiwa kutoka Marekani huku barani Ulaya ina nusu ya wagonjwa.

Siku ya Alhamisi Uhispania ilisema watu 950 wamepoteza maisha katika kipindi cha saa 24, na Marekani iliorodhesha 1,000 katika kipindi hicho.

Idadi ya watu waliothibitishwa kuambukizwa nchini Uhispania ilipanda kutoka 102,136 siku ya Jumatano kufikia 110,238, kiwango hicho sawa na asilimia 8 za siku zilizopita.

Mamlaka zinaamini inatarajia kushuhudia idadi ya wanaoambukizwa ikishuka siku za mbele.

*BBC*




Polisi waliovaa kofia zinazofanana na virusi vya corona, wakitoa malekezo kwa wachuuzi jinsi ya kukaa hatua na mwingine, baada ya serikali kuondoa amri ya kukaa majumbani katika mji wa Chennai, China juzi. **(PICHA: AFP)**

# WHO yaonya mataifa Mashariki ya Kati

**ISALAMABAD, Pakistan**

SHIRIKA la Afya Duniani, limezitaka nchi za Mashariki ya Kati kuchukua hatua za haraka kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona.

Tamko hilo limetolewa baada ya kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa kufikia 60,000, ikiwa ni mara mbili maambukizi .

Mkurugenzi wa shirika hilo Mashariki mwa Mediterenia, ikijumuisha Pakistan, Afghanistan, Somalia na Djibouti na mataifa mengine, Ahmed Al-Mandhari, amesema kuwa wagonjwa wapya wameripotiwa katika baadhi ya maeneo dhaifu zaidi katika mataifa hayo.

Mandhari alisema kuwa hata katika mataifa yalio na mifumo bora ya afya, kumekuwa na ongezeko na kutia wasiwasi.

WHO imesema idadi kamili ya maambukizi katika eneo hilo, iliongezeka kufikia 58,168 kutoka 32,442 mnamo March 26, mwaka huu.

*DW*

## Chanjo corona kufanyiwa majaribio

**SYDNEY, Australia**

WANASAYANSI nchini Australia, wameanza kufanya majaribio ya dawa mbili zinazoweza kuwa chanjo dhidi ya virusi vya corona.

Hatua hiyo inatajwa kuwa muhimu katika majaribio ya kimaabara.

Chanjo hizo zilizotengenezwa na Chuo Kikuu cha Oxford na kampuni moja ya Marekani ya madawa ya Inovio Pharmaceutical.

Shirika la Afya Duniani (WHO) imeidhinisha kufanywa kwa majaribio jayo kwa kuwatumia wanyama.

Shirika la Sayansi la Taifa nchini Australia, litatathmini kama chanjo hizo zinafanya kazi na kama salama kwa binadamu.

Majaribio ya kwanza kwa binadamu yalifanyika nchini Marekani mwezi uliopita.

Kuna chanjo nyingine kadhaa zinazofanyiwa uchunguzi katika maeneo mbalimbali duniani.

Wanasayansi wa Jumuiya ya Madola na Shirika la Utafiti wa kisayansi (CSIRO) Australia, walisema vipimo vyao vitakuwa vya kwanza vilivyokamilika kwa kuwatumia mnyama kabla ya kupewa binadamu.

Watafiti wanasema haikutarajiwa kuwapo kwa kasi na kiwango cha ushirikiano unaonyeshwa sasa.

"Kwa kawaida inaweza kuchukua takriban mwaka mmoja hadi miwili kufikia hapa tulipo, kusema ukweli tumefupisha kipindi hicho hadi miezi," Dk. Rob Grenfell kutoka CSIRO amewaambia waandishi.

**BBC**

**Shirika la Sayansi la Taifa nchini Australia, litatathmini kama chanjo hizo zinafanya kazi na kama salama kwa binadamu.**

# Kenya wasimamisha polisi walioua raia

**NAIROBI, Kenya**

SERIKALI ya Kenya imechukua hatua ya kuwasimamisha kazi polisi wanaotuhumiwa kuhusika watu waliokiuka amri kutotoka nje.

Idara ya usalama ya nchi hiyo, imetangaza polisi wanne wamesimamishwa kazi wakisubiri uchunguzi kuhusu tukio hilo.

Wakati hatua hiyo imechukuliwa, watu wengine wawili wameuawa katika maeneo ya Kakamega na Kwale.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Bonde la Ufa, Marcus Ocholla, amethibitisha kupokea ripoti kadhaa kuhusu maofisa wa polisi kuwajeruhi raia.

Katika muda wa wiki moja sasa, kumeongezeka matukio ya polisi kutumia nguvu kupita kiasi.

Mjini Busia zaidi ya watu 10 wamejeruhiwa na kulazwa hospitali baada ya polisi kuingia kwa nguvu katika nyumba moja ambayo watu walijifungia baada ya saa za kutembea kumalizika.

*DW*

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.
Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

# Mauaji Harusini-7

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




Kilichokuwa sasa kinasubiriwa ni simu tu kutoka kwa Kidaga ili amalize mchezo. Kabla hajamaliza kufikiria, simu akamtetemesha kwenye suruali. Hakuna ameweka mlio. Aliitoa na kuitazama. Ilikuwa ni ya Kidaga. Aliiweka sikioni.

"Tayari, muda umefika." Ilikuwa ni amri. Wakati huo maharusi walikuwa wamebakisha mita chache kufika kwenye eneo ambalo limetengenezwa maturubai ya kisasa kabisa kwa ajili ya sherehe hizo.

Aliminya kitufe cha simu, akaihamisha mkono wa kushoto. Mkono wa kulia, ulirudi kwenye mfuko wa nyuma na kuigusa bastola. Lakini hakuitoa. Aliona kuna kitu hakiko sawa. Akaiingiza simu mfukoni kwa mkono wa kushoto, lakini kwenye mkono huo huo, akatoa leso ya kufutia jasho.

Leso ile na mkono wa kushoto ukahama kuelekea upande wa kulia. Akatoa bastola kwa mkono wa kulia na haraka kama umeme, akagusanisha mikono yote, hivyo kastola yake ndogo ikawa imefumbatwa na leso. Haikuonekana na mtu yoyote.

Aliinua mkono wa kulia juu ambao ulionekana kuwa alikuwa ameshika leso kwa ajili ya kujifutia jasho kutokana na joto.

Alisogeza leso kidogo mbele na kuivuta kwa nyuma ili kupatikana na uwazi mbele na kupiga risasi. Alianza kumlenga bwana harusi kwenye paji la uso kwa sababu alikuwa mbele yao. Aliachia risasi moja tu ambayo haikukosea, badala yake ikaenda pale pale ilipokusudiwa. Bwana harusi aliyumba kama mlevi, kabla ya kuanguka chini taratibu.

Ni kitendo bila kuchelewa, kwani wakati watu hajajui nini kinaendelea, aliachia nyingine kwenye paji la uso la bi harusi. Yeye alianguka kama mzigo, akimlalia mumewe.

Hakutaka kujisumbua kama ameshaua au la. Kutokana na uzoefu wake risasi ya paji la uso alizokuwa akizipiga siku zote ziliwaua majambazi hatari na wakorofi, wenye roho mbaya zaidi ya shetani, achilia mbali bwana na bi harusi ambao hawajawahi kuua hata kuku.

Upesi yeye na Michael Sabuni walikwenda kwenye gari alilokuwa akiendesha Tofiki Seif , pembeni yake kukiwa na Kidaga na kuondoka kwa kasi.

"Bosi, tumemaliza kazi uliyotutuma, kwa sasa tunakuja kwako ili tumalizie mzigo uliobaki." Kidaga akimtaarifu Abeshi."

*******************************************

Hakuna yoyote aliyezungumza ndani ya gari lililokuwa likienda kwa kasi kana kwamba liko kwenye mashindano.

Tofiki Seif alikuwa kwenye usukani, akiitafuna lami na lami ikamtii. Kuna wakati aliowabeba Kidaga, Michael na Tamim waliingia woga kutokana na kasi ambayo haikuwa ya kawaida. Lakini kila mmoja alibaki kuugulia kimoyomoyo.

Kutoka Kibada, hakutaka kupitia barabara ya daraja la Kigamboni kama walipokuja.

Badala yake walipita barabara inayotoka Kibada, kwenda Maliasili, Mikwambe, Tuangoma hadi Kongowe.

Tofiki aliona njia hiyo itakuwa ni salama zaidi kuliko ya kwanza kwenda hadi Kigamboni na kusubiri kivuko.

Njia hiyo kwao ilikuwa ni hatari zaidi kuliko hatari yenyewe, kwani wanaweza kukamatwa wakiwa wanasubiri kivuko au ndani ya kivuko chenyewe.

Ya pili ambayo nayo Tofiki hauiona nzuri sana ni ile waliojia na msafara wa harusi. Ni ile ya darajani. Mwanzo na mwisho wa daraja kuna vizuizi ambavyo vingekuwa ni vikwazo vizuri kwa wao kutiwa mbaroni.

Ya tatu ndiyo ilionekana salama. Haikuwa na vikwazo, lakini pia ilikuwa wazi zaidi isiyokuwa na foleni kama ilivyo kawaida ya barabara hiyo ya Kigamboni hadi Kongowe.

Gari ilipofika Kongowe, ilikata kulia kuelekea Mbagala na huko tayari walijiona wako salama.

Hakuna yoyote aliyeweza kuliona gari hilo likiondoka eneo hilo kwa kasi, kwa sababu kila mmoja alikuwa kwenye harakati ya kuponyesha maisha yake.

Walifika salama Mbweni jijini Dar es Salaam na gari lao kuruhusiwa kuingia kwenye geti la nyuma ya Abesh.

****************************************

"Kazi nzuri vijana. Kwa sababu pamoja na Kidaga kuniambia kuwa imekwisha, lakini dakika tano zilizopita nilikuwa namuona Kamanda wa Polisi Kanda Maalum akitangaza rasmi kutokea mauaji ya bwana na bibi harusi maeneo ya Kibada jijini Dar es Salaam.

Ina maana tayari imethibitishwa kama wote wamekufa na ndicho nilichokuwa nikitaka, hongereni sana vijana." Abesh aliwapongeza vijana wale wanne, Tamim, Michael, Tofiki na Kidaga.

Waliitikia kwa heshima, lakini akili yao ilikuwa kwenye pesa yao iliyobaki. Ni kwamba awali walipewa nusu malipo, pamoja na pesa ya ziada ambayo ingeweza kutumika pale lolote au chochote ambacho kingetokea kwenye tukio.

Walikuwa wamekaa kwenye kochi lile lile ambalo siku ya kwanza walikuwa wakipeana mikakati ya kufanya mauaji hayo.

Abesh, aliingia ndani na kukaa kiasi cha dakika 10 hivi, akatoka na bahasa nne za khaki, zilizokuwa na majina ya wote wanne waliokuwa pale. Kila mmoja akampatia bahashayake.

"Hesabuni ili mhakikishe." Baada ya kila mmoja kuhakikisha kuwa pesa yake ya malipo za ziada iko kamili, Abesh aliunguruma tena.

"Tumemaliza kazi. Lakini tukumbuke kuwa polisi nao wameanza kazi. Hivi itabidi tujichunge nyendo zetu. Kama kawaida, najua watu wa kazi kawaida yao ni kwamba ikitokea bahati mbaya mmoja akikatwa hatotaja wenzake, wala mfadhili ya tukio hilo, sawa jamani?" Aliuliza. Wote waliitikia kukubali.

Hakuwa na wasiwasi sana kutokana na kwamba watu hao walionekana kuwa ni wazoefu na hatari kwa matukio kama hayo, hivyo wanajua kila kitu na wameshafanya matukio mengi na hadi leo bado anadunda na kuzidi kupotea tenda mbalimbali na kufanya matukio kama hayo.

"Bosi tumekusikia na sisi tumemaliza kazi kwako, haya mengine tuachie, sisis ndiyo kazi yetu, hutosikia chochote. Na kuanzia sasa, mimi na wenzangu wote tutatoka humu kwako mmoja mmoja kwa nyakati tofauti na kila mmoja ataondoka kivyake na atakwenda kutafuta usafiri mbele ya safari, sawa jamani? Tamim aliwataarifu wenzake nini kinafuata baada ya hapo.

Kimoyomoyo, Abesh alionekana kuwahusudu jamaa wale kutokana na jinsi wanavyoweza kutekeleza kazi na pia kujilinda.

Akiwa peke yake ndani alikuwa akijipongeza kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kumuua Patiyo na mkewe Grace.

Patiyo, rafiki yake mkubwa kwenye masuala ya biashara kumgeuka na kumchukua mpenzi wake ambaye alitarajia kumuoa ni kitendo ambacho alikiona ni cha kumdhalilisha mtu kama yeye ambaye ni milionea na mwenye heshima kubwa nchini.

Alimkumbuka Grace, msichana aliyekuwa anampenda. Roho ilimuuma kiasi kutokana na mapenzi aliyokuwa nayo juu yake, lakini hakuwa na la kufanya, kwani kitendo cha kumgeuka na kuanza uhusiano wa kimapenzi na rafiki yake, alikiona ni cha kisaliti, kumtia aibu na ukosefu wa adabu.

"Sikutaka kumuua, lakini umenilazimisha nifanye hivyo Grace. Nilikupenda sana, lakini hukuujali upendo wote juu yangu." Alijikuta akiongea peke yake.

Alikwenda kwenye friji na kutoa vitoti vitatu vya pombe kali, anavimimina kwenye glasi. Akachukua pia kidonge cha barafu na kutia kwenye glasi iliyokuwa na pombe. Akakaa kwenye kochi. Akainyanyua na kupiga mafunda kadhaa, miguu yake ikiwa mezani. Ilikuwa ni siku ya kufuahia ushindi wake, baada ya kukaa na sononeko kwa muda mrefu.

Yeye ni tajiri, hawezi kuchukuliwa demu na kuanza kulialia kama mtu ambaye hana mbele wala nyuma. Ni lazima afanye kitu. Alipize kisasi kama alivyofanya. Usingizi mzito ukampitia.

***Itaendelea Jumamosi***

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES**

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

### NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyuma kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:


### PIKIPIKI IMEIBIWA



Ndugu Peter Masawe mwenye picha hapo juu ameiba pikipiki yenye namba za usajili MC 343 BZQ Boxer na kadi original namba 7833925 ya pikipiki.

Yeyota atakayemuona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu au apige simu namba 0658112243.

**Zawadi nono itatolewa.**

Taarifa ya polisi:

**BUG/RB/8287/2019.**

115689702

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE HIGH COURT OF TANZANIA)**
**AT ARUSHA**
**MISC.LAND APPLICATION NO 72 OF 2018**
**(C/F Court Land Appeal No. 27 of 2017, Originated Karatu District Land and Housing Tribunal Application No. 22 of 2008)**
**JOSEPH LOHAY AKUNAAY ………………APPLICANT**
**VERSUS**
**PASKALI CLETI MAGHWAY…………………RESPONDENT**

**NOTICE OF HEARING**

TO: PASKALI CLETI MAGHWAY.
ARUSHA

**TAKE NOTICE** that the above appeal has been fized forHearing on 23rd day of April 2020 at 9:00o'clock, at High Court –Arusha.
YOU may appear in person or through your Advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time, the Court may proceed to hear the application and pronounce Ruling in your absence.
GIVEN under my HAND and the SEAL of the COURT this 19th day of March,2020.

J. F. NKWABI
DEPUTY REGISTRAR
ARUSHA

115689902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo:**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;93/2020**

Ombi la **SHABANI OMARY MASENGA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **HABIBA OMARY DIKULAGWA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 22/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/04/2020.

MOROGORO

1568961

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

MBAROUK KHAMIS MBAROUK anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 692 AWH NISSAN MARCH.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
TAN/RB/282961/2020.

115690302

---


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# PSG yajiunga na Chelsea,Juve kumwania Hakimi

**PARIS, Ufaransa**

MIAMBA wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain imeripotiwa kujiunga kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Real Madrid, Achraf Hakimi kipindi cha majira ya joto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Morocco anatarajiwa kurudi pale kwenye dimba la Bernabeu wakati mkataba wake wa mkopo wa miaka miwili na Borussia Dortmund utakapomalizika.

Miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wanataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, huku Chelsea na Juventus pia zikihusishwa kumwania.

Hakimi, ambaye anauwezo wa kucheza nafasi zote za ulinzi, lakini akipendelea zaidi kucheza beki ya kulia, amekuwa na kiwango cha kuvutia pale Borussia Dortmund.

Akiwa ni zao la akademi ya vijana ya Real Madrid, Hakimi ni mchezaji wa kimataifa wa Morocco ambaye ameichezea nchi yake mechi 28.

Hakimi amecheza mechi 17 kwa Real na alikuwa kwenye kikosi hicho wakati wakishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2017-18.

Mwaka 2018, Hakimi alijiunga na Dortmund kwa mkopo wa miaka miwili na amejiimarisha kwenye kikosi hicho kwa kuonyesha kiwango cha kuvutia.

Mkataba wa sasa wa Hakimi pale Real Madrid unamalizika kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2022.

## WILLIAMS ATAJWA KUTUA UNITED

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imesitisha mchakato wa kusaka beki wa kushoto mpya baada ya kuridhishwa na kiwango cha Brandon Williams, limeandika gazeti la The Sun.

Chanzo cha habari kutoka Old Trafford kimeliambia gazeti hili kuwa : 'Kocha amemweleza Brandon kuendelea kufanya anachokifanya na kuendelea kujiimarisha anapokuwa uwanjani.

"Kwa wakati huo huo, Ole ameacha kuendelea kusaka beki wa kushoto mpya. Inaonekana ameridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na Brandon.

" Inaonekana kuna uwezekazo anaweza kuondoka kama alivyofanya Dean Henderson, kujiunga na klabu nyingine ya Ligi Kuu England au timu nyingine inayoshiriki Ligi ya Championship.

"Ole anapenda mwonekano na tabia ya Brandon, anatarajiwa kuwa hapa katika msimu ujao. Mabosi wanaamini wataokoa pauni milioni 50."

Williams ameonekana kuwa katika mawindo tangu kuanza kwa msimu huu huku kikosi cha Ole Gunnar kikipata matokeo yasiyoridhisha.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 19 amekuwa ni shabiki wa klabu hiyo ya Old Trafford na amemfanya Luke Shaw kuwa nje ya kikosi.

Inaelezwa kuwa Williams amekuwa katika mazungumzo na Solskjaer katika wiki chache zilizopita kujadiliana juu ya hatima yake.

Williams alisaini mkataba mpya na klabu yake kabla ya Krismasi ambao utamweka klabuni hapo hadi mwaka 2022 lakini kukiwa na kipengele cha kuongeza cha miezi 12.

# Dier aepuka adhabu kwa kumvaa shabiki

LONDON, England

NYOTA wa Tottenham Hotspurs, Eric Dier, hatachukuliwa hatua yoyote na polisi baada ya kumvamia shabiki jukwaani ili apigane nae wakati timu yake ikiambulia kichapo kutoka kwa Norwich City kwenye mchezo wa Kombe la FA.

Dier alimrukia jukwaani shabiki na kumvaa ili apiganae nae baada ya kuwashutumu wachezaji wa Tottenham wakati wa mchezo huo.


Polisi walilazimika kufanya uchunguzi wa kina wa kurudi kuliangalia tukio hilo kwenye video na wametoa taarifa kwamba: "Uchunguzi umekamilika na hakuna hatua zozote zitakazochukuliwa dhidi ya mchezaji."

Chama cha Soka cha England, FA, kilianzisha uchunguzi wa tukio hili mara baada ya mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur mwezi uliopita.

Kiungo huyo alionekana kuwa na hasira kali baada ya kaka yake kuhusika kwenye ugomvi na shabiki mmoja ambaye alionekana kumtukana mchezaji huyo.

Mashahidi walielezea kwamba, matusi na kashfa zilizokuwa zinatolewa na mashabiki waliokaa jirani na kaka wa Dier dhidi ya wachezaji wa Spurs ndio yalimkasirisha mchezaji huyo.

Awali kocha wa Tottenham, Jose Mourinho, alisema kwamba mchezaji huyo hakupaswa kuchukua hatua alizochukua, badala yake angepuuzia na kubakia uwanjani.



## HABARI MICHEZO



# MODRIC

## KUMALIZIA MKATABA WAKE MADRID

**MADRID, Hispania**

LUKA Modric anapanga kuendelea kukaa pale Real Madrid hadi mkataba wake utakapomalizika mwaka 2021, kwa mujibu wa ripoti za nchini Hispania.

Kulikuwa na taarifa kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 anaweza kuondoka klabuni hapo ili kuwapisha vijana wanaochipukia akiwamo Martin Odegaard, ambaye amekuwa na mafanikio makubwa kule Real Sociedad anakocheza kwa mkopo.

Na Modric ameliambia benchi la ufundi la klabu ya Real kwamba angependa kumalizia muda wake uliobaki kwenye mkataba wake klabuni hapo.

Gazeti la AS la nchini Hispania limeripoti kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia, ameamua kubakia hapo kwa msimu ujao licha ya kuwaniwa na klabu kadhaa.

Modric msimu huu umekuwa mgumu kwake, kwa kushindwa kuonyesha kiwango chake dimbani.

## Spurs kumpunguzia Mourinho bajeti ya usajili

**LONDON, England**

TOTTENHAM inapanga kupunguza bajeti ya usajili ya Jose Mourinho ikiwa ni tahadhari ya mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Spurs imefikia uamuzi huo kutokana na athari ya ugonjwa huo ambao umekuwa pigo kubwa kwao kwa kutoingiza kiasi cha fedha ambacho walikitarajia msimu huu.

Tottenham pia inapanga kupunguza mishahara ya wachezaji wake pamoja na wafanyakazi wa klabu hiyo ikiwa ni sehemu ya kujinusuru kutokana na janga hilo ambalo limeathiri kwa kiasi kikubwa sekta ya michezo.

Gazeti la Daily Mail limebainisha kwamba, Spurs wamefikia hatua hiyo ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha shughuli nyingine ndani ya klabu hiyo ziweze kuendelea kama ilivyo kawaida.

Mourinho, pamoja na mwenyekiti wake, Daniel Levy na Ofisa Mkuu, Steve Hitchen, tayari wameshajadiliana kuhusu mipango ya usajili wa dirisha kubwa na vipaumbele walivyoviweka.

Kwa mujibu wa Dail Mail, Spurs kwenye usajili ujao imeangalia nafasi zenye upungufu ambazo ni mlinzi wa kati, beki wa pembeni na mshambuliaji wa kati ndio sehemu ambazo zitawafanya waingie sokoni ili kuziimarisha.



# Del Piero ampigia debe Dybala unahodha Juve

**TURIN, Italia**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Juventus, Alessandro Del Piero, anaamini Paulo Dybala amepevuka zaidi katika klabu hiyo msimu huu baada ya sakata la uhamisho lililomtingisha kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alikuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na miamba wa Ligi Kuu England, Manchester United na Tottenham, lakini uhamisho wake ulishindikana.

Na Del Piero, ambaye aliichezea Juventus kwa kipindi cha miaka 19, amesisitiza kwamba, Dybala ameimarika zaidi tangu kipindi cha majira ya joto kilichopita na anaweza kuwa nahodha wa klabu hiyo siku moja.

"Paulo tayari ameshaonja kitambaa cha unahodha mara chache na kama hilo limeshatokea wanaweza kumfikiria kwa siku zijazo," amesema Del Piero akiiambia Sky Sport Italia. "Kwa namna ninavyomjua yeye binafsi, naamini kupevuka kwake kumemfanya akue zaidi, hasa kutokana na namna alivyochukulia sakata lake la uhamisho kipindi cha majira ya joto kilichopita, ambalo lilimwonyesha amekua.



"Amekuwa akijituma na kuipigania klabu na nafikiri amekamilika kwa heshima pia."

Kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona, Dybala alikuwa kwenye kiwango bora.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 amefunga mabao 13 na kutoa asisiti 12 katika mechi 34 alizoichezea Juventus msimu huu.

Dybala alikuwa mchezaji wa tatu wa Juventus kukutwa na ugonjwa wa corona mwezi uliopita baada ya Daniele Rugani na Blaise Matuidi.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# JIMENEZ AZIITA UNITED, MADRID

●●●Mshambuliaji huyo afunguka tayari ameiva kwenda kupambana kwenye klabu hizo...

**LONDON, England**

RAUL Jimenez amebainisha kwamba hakuna kifungu cha fedha cha kumruhusu kuondoka kwenye mkataba wake na Wolves, huku klabu kadhaa zikionyesha nia ya kuwania kumsajili kutoka pale kwenye dimba la Molineux.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Mexico alikuwa mmoja wa nyota waliong'ara kwenye Ligi Kuu England msimu huu kabla ya kusimamishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona, akifunga mabao 22 katika mashindano yote.

Klabu za Manchester United na Real Madrid zimekuwa zikimtolea macho Jimenez ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2023.

Amesema: "Namna wao (Wolves) walivyoninunua mimi kwa euro milioni 40, hawataniuza kwa bei pungufu. Hakuna kipengele cha fedha za kuniuza, lakini klabu za England uendeshaji wao uko tofauti sana."

Jimenez pia amesema kwamba, kabla hajajiunga na Wolves, wakati akicheza kule Benfica, alipewa ofa ya kulipwa mshahara wa pauni milioni 6.9 baada ya makatato ya kodi ili ajiunge na klabu ya Ligi Kuu China.

Aliikataa ofa hiyo kwa sababu alikuwa bado ana nia ya kuendelea kujiimarisha yeye mwenyewe kwenye ligi ngumu duniani.

Jimenez ameliambia gazeti la Marca la nchini Hispania: "Nafikiri ulikuwa mshahara wa euro milioni 8 (sawa na pauni milioni 6.9) kwa mwaka.

"Lakini unatakiwa kufikiria vitu vyote viwili kwa pamoja, namna unavyoweza kuendelea kipaji chao na kufanikiwa kwenye mashindano makubwa pamoja na kiasi cha fedha.

"Uamuzi niliochukua ni kubakia pale Benfica, halafu nikafanya uamuzi wa kuja hapa Wolves, licha ya kuwa ilikuwa ndio imepanda daraja, watu wote walijua kwamba tutakuwa tukipambana kutoshuka daraja, tulikuwa na msimu mzuri na tukafuzu kucheza michuano ya Europa."

## KWA UFUPI

**GREALISH AOTA MBAWA**
KIUNGO wa Aston Villa ambaye ni raia wa England, Jack Grealish (24), ameelezwa hana nafasi ya kujiunga na Manchester United katika majira ya joto. ***(Star)***

**WILSON ASHANGAZWA**
STRAIKA wa Bournemouth, Callum Wilson (28), amesema hastahili kuwindwa na klabu kubwa zinazoshiriki Ligi Kuu England kwa sababu ya kiwango kibovu alichokionyesha msimu huu. ***(Sky Sports)***

**DAVID AITAMANI EPL**
MSHAMBULIAJI wa Gent na Timu ya Taifa ya Canada, Jonathan David, ambaye ana umri wa miaka 20, amesema anapenda kuona hapo baadaye anajiunga na klabu yoyote inayoshiriki Ligi Kuu England. ***(Guardian)***

**AUBAMEYANG, SANE WATATA**
STRAIKA wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang (30), na winga wa Manchester City, Leroy Sane (24), ni baadhi ya wachezaji wanaoziumiza 'vichwa' klabu zao kutokana na kutokamilika kwa mazungumzo ya kusaini mikataba mipya baada ya dirisha la usajili kukaribia. ***(Telegraph)***

**HAKIMI AGOMBEWA**
Paris Saint-Germain imeingia katika vita ya kuwania saini ya beki, Achraf Hakimi (21). Juventus pia inatajwa kumwinda nyota huyo ambaye yuko mkataba wake wa mkopo Borussia Dortmund unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu. ***(Mail)***

**CEBALLOS NJIA MOJA**
KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Ceballos (23), amewekwa katika orodha ya wachezaji ambao watatolewa na Real Madrid kama sehemu ya kufanikisha mchakato wa kujiunga na Arsenal. ***(Mirror)***

**LOPEZ ANUKIA VILLA**
ASTON Villa inatajwa kuanza mchakato wa kumsajili kiungo wa Marseille ya Ufaransa, Maxime Lopez, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Birmingham Live)***

**SON AMALIZA MAFUNZO**
MSHAMBULIAJI wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Korea Kusini, Son Heung-min (27), anakaribia kukamilisha mafunzo ya wiki nne ya jeshi nchini mwake aliyoyafanya katika muda huu ambao ligi mbalimbali zimesimama kufuatia kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. ***(Sun)***

**BRUYNE ATOA ANGALIZO**
KIUNGO Mbelgiji wa Manchester City, Kevin de Bruyne (28), anaonya uwezekano wa kupata wachezaji wengi majeruhi endapo mamlaka zinazosimamia soka zitaamua mechi za ligi kuanza mapema. ***(Telegraph)***

**RODRIGUEZ AOMBA DUA**
MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (28), amesema atafurahi kuona anaungana tena na kocha wake wa zamani Carlo Anceloотti. ***(Mirror)***

**PEREIRA AIOTA EPL**
KIUNGO wa Manchester United, Andreas Pereira, amejiandaa kucheza mechi zilizobakia za Ligi Kuu England ili kukamilisha msimu huu mapema iwezekanavyo. Msimu wa 2019/20 umesimama katika mataifa mbalimbali kutokana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona ***(COVID 19).***

HABARI MICHEZO

# MWAMBUSI AFUNGUKA MAKOCHA WAZALENDO WANAVYODHARAULIWA

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Kocha Msaidizi wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema makocha wazalendo wamekuwa na changamoto ya kutofanya vizuri katika timu mbalimbali wanazofundisha hapa nchini kwa sababu ya kutotimiziwa mahitaji yao kikamilifu.

Akizungumza katika mahojiano maalumu jijini Dar es Salaam jana, Mwambusi alisema timu haziwezi kupata matokeo mazuri kama mahitaji ya benchi la ufundi yatashindwa kutekelezwa kwa asilimia 100.

Mwambusi, kocha huyo wa zamani wa Tanzania Prisons na Mbeya City za jijini Mbeya, alisema changamoto hiyo imewafanya makocha wengi kuonekana uwezo wao ni mdogo, jambo ambalo si kweli.

Kocha huyo alieleza endapo kocha mzalendo akaomba kupatiwa mipira 100 kwa ajili ya mazoezi, hawezi kupewa lakini klabu hiyo hiyo ikiwa chini ya mwalimu kutoka nje ya nchi akihitaji mipira kwa idadi kama hiyo, atapewa mia 200 au 150.

Aliongeza kuwa anajivunia alipokuwa Azam FC kwa kushirikisha na Mholanzi Hans van de Pluijm walipata mafanikio licha ya mikataba yao kusitishwa ndani ya muda mfupi.

"Sisi tumekabidhiwa ofisi tutakapa mafanikio, tumeondoka pale tukiwa tumeacha makombe mawili, sisi ni washindi, siwezi kusema kama tumefeli, labda baada ya kuondoka sisi wamepata makombe mangapi," alihoji Mwambusi.

Kocha huyo alisema walipokuwa Azam FC hawakugawa wachezaji na walitoa nafasi ya nyota kucheza kutokana na nidhamu yao waliyokuwa wanaionyesha.

"Kuna wachezaji walikuwa wanafika mazoezini baada ya dakika 10 mazoezi kuanza, kuna wachezaji walikuwa wanauwezo wa kwenda 'kujikosha' kwa viongozi, sasa kilichoonekana kama tulitengenezewa 'bomu' kuelekea mechi dhidi ya Simba ambayo tulifungwa," Mwambusi alisema.

Aliongeza makocha wa Tanzania wanashindwa kwenda kufundisha nje ya nchi kwa sababu hapa wanapata maslahi bora zaidi na yeye aliwahi kukataa ofa ya kufundisha Rwanda kwa sababu dau alilopewa halikuwa lakuvutia.



Beki wa Azam, Nico Wadada (kulia), akimtoka mchezaji wa KMC FC, Amos Kadikile, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Islam, Batenga mabosi wapya Yanga

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umetangaza kuwateua wanachama wawili, Suma Mwaitenda na Haruna Batenga, kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo ili kuziba nafasi zilizoachwa na viongozi wengine waliojiuzulu hivi karibuni, imefahamika.

Shija Richard, Said Kambi na Rogers Gumbo walitangaza kujiweka pembeni kwa madai wanawapa nafasi wengine kuendelea kuitumikia Yanga ambayo ni taasisi kubwa kuliko wao.

Taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli imesema viongozi hao wameteuliwa na kupata baraka na Kamati ya Utendaji ya Yanga iliyokutana chini ya Mwenyekiti, Mshindo Msolla.

Bumbuli alisema pia kamati hiyo imemteuwa Hamad Islam kuwa Mwenyekiti mpya wa Kamati ya Mashindano na Dominic Albinus atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundi.

Machi 27 mwaka huu Yanga ilitangaza walijiuzulu huku wawili wakiondolewa kwenye madaraka yao na kupelekwa katika Kamati ya Nidhamu ya klabu hiyo.

Viongozi waliosimamishwa ni pamoja na Salim Rupia na Frank Kamugisha.

Hata hivyo upepo ndani ya klabu hiyo bado haujatulia kutokana na baadhi ya viongozi kutokubaliana na shughuli za kiutawala zinazofanywa na wadhamini wao, Kampuni ya GSM.

# Chupikizi yalia kukosa bahati

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

UONGOZI wa Chipukizi inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar umesema kufanya vibaya kwa timu hiyo hakutokani na usajili 'mbovu' waliofanya ambao umeshindwa kupambana na kasi iliyopo katika ligi hiyo msimu huu.

Timu hiyo yenye makazi yake Kisiwani Pemba inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi tisa baada ya kushinda mchezo mmoja, sare mechi sita na kufungwa michezo sita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa timu hiyo, Ali Khamis, alisema walisajili wachezaji wenye uzoefu lakini matokeo ya mpira hayakuwa mazuri kwa upande wao tangu kuanza kwa msimu.

Khamis alisema timu hiyo ilijitahidi kufanya maandalizi ya mapema ya msimu licha ya kuikabiliwa na ukata wa fedha lakini wamekuwa wakiambulia matokeo mabaya kila wanaposhuka dimbani.

Alisema msimu huu kumekuwa na upinzani na ushindani na katika kila mechi timu zote zimekuwa zikipambana kusaka ushindi hali iliyopelekea wao kuburuza mkia.

**" Mpira ni mchezo wa makosa, ukitoa nafasi kidogo lazima mpinzani wako ataitumia nafasi hiyo, makosa madogo madogo ya kiuchezaji ndiyo yanapoteza matokeo, naamini msimu huu mpira kwa upande wetu umetukataa," alisema kiongozi huyo.**

Aliongeza hawajakata tamaa sasa hivi wanajiimarisha ili ligi itakaporejea tena wapambane na kuhakikisha hawashuki daraja.

# Simba yashtukia 'wapiga mizinga'

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba ya jijini Dar es Salaam, imesema haijatoa mamlaka kwa mtu yoyote kuingia makubaliano au mikataba kwa niaba ya klabu hiyo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mbatha alisema jana mikataba na makubaliano yoyote yanayoihusu klabu hiyo ni lazima yasainiwe katika ofisi za mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara na si mahali kwingine.

"Imefahamika kuwa kuna baadhi ya watu, makundi ya watu wamekuwa wakiingia makubaliano, mikataba na taasisi, kampuni nyingine wakijiwasilisha kama wafanyakazi, wawakilishi wa Kampuni ya Klabu ya Simba,"alisema Mbatha.

Mbatha alisema klabu inatoa rai kwa umma kuchukua tahadhari na watu au makundi ya watu wanaojitambulisha kama wafanyakazi au wawakilishi wa klabu kwa ajili ya manufaa yao binafsi.

"Simba inakemea vikali vitendo vya namna hii na inaomba wananchi kutoa taarifa za watu au makundi ya watu wa namna hii kupitia ofisi ya Mtendaji Mkuu,"Mbatha aliongeza.

Simba sasa inaongozwa na Bodi ya Wakurugenzi iliyoko chini ya Mwenyekiti, Mohamed Dewji 'MO', Salim Abdallah, Hussein Kitta, Dkt. Zawadi Kadunda, Suleiman Haroub, Asha Baraka na Mwina Kaduguda.

# Michezo

Jumamosi Aprili 4, 2020

Nipashe




## Jimenez aziita United, Madrid

HABARI UK 30



Kiungo wa Yanga, Papy Tshishimbi (kushoto), akiwa na mshambuliaji wa timu hiyo, David Molinga, katika moja ya mechi za Ligi Kuu Bara. Nyota hao wawili wote ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). **PICHA: MAKTABA**

## Tshishimbi, Yanga sasa kimeeleweka

**Na Saada Akida**

BAADA ya majadiliano ya zaidi ya wiki moja kufanyika, kiungo wa kimataifa wa Yanga kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Papy Tshishimbi anatarajiwa kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo ya jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Taarifa zilizopatikana jijini jana kutoka ndani ya Yanga zinasema kuwa tayari kikao cha kukamilisha mazungumzo kimeshafanyika na kukubaliana kiungo huyo atasaini mkataba wa miaka miwili.

Chanzo chetu kilisema kikao hicho kilimhusisha mchezaji husika, viongozi wa klabu pamoja na wadhamini wao, Kampuni ya GSM.

"Baada ya kufanya mazungumzo ya muda mrefu na Tshishimbi, tumemalizana nae jana (juzi ) na makubaliano yetu kuongezewa mkataba yatafanyika kesho (leo), na atasaini mkataba wa miaka miwili ya kuitumikia Yanga," kilisema chanzo chetu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Tshishimbi, alisema anasubiri kuitwa na mabosi wake ili kwenda kukamilisha mchakato huo wa kusaini mkataba mpya.

"Nimeongea na mabosi wa Yanga, kiukweli mazungumzo yameenda vizuri na sasa nasubiri simu yao ya kuniita ili nikasaini mkataba mwingine kuendelea kuitumikia Yanga, hicho ndicho kinachoweza kukueleza" alisema nahodha huyo.

Mkataba wa sasa wa kiungo huyo ndani ya Yanga umebakisha miezi minne na klabu yake inajipanga kukamilisha mchakato huo baada ya kuwapo kwa tetesi za kutakiwa na watani zao, Simba.

# SIMBA YAIKEBEHI YANGA

●●● Ni kuhusu uamuzi wa kufuta msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa mwaka 2019/20, TFF yasisitiza kusubiri mwongozo wa Serikali...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI bado Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), ambayo iko chini ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF), haijatoa taarifa mpya kuhusiana na hatima ya Ligi Kuu Bara, uongozi wa Simba umewashangaa watani zao kwa kupendekeza msimu wa 2019/20 ufutwe.

Ligi Kuu Tanzania Bara ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kufuatia agizo la serikali la kusimamisha ligi zote ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

Simba yenye pointi 71 na inahitaji pointi 12 tu ili itetee taji hilo, ndio vinara wa ligi hiyo ya juu inayosimamiwa na TFF na hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mbali na ligi hiyo, ligi nyingine zilizosimama hapa nchini ni pamoja na Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili, Ligi Kuu ya Wanawake na mashindano ya Kombe la FA, ambayo hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema anasikitishwa na kauli 'nyepesi' kutoka kwa viongozi wa Yanga ambao wanashauri ligi hiyo ifutwe wakati zilikuwa zimebakia mechi chache.

Manara alisema kama Ligi Kuu Bara itafutwa, mwakilishi wa nchi katika mashindano ya kimataifa atapatikana kwa mfumo gani ambao hautaleta malalamiko.

"Kwa hiyo ligi ikifutwa (jina la utani), ndio mtakuwa mabingwa?, Hivi tunafikiri vizuri kweli? Kwa hiyo timu gani itawakilisha nchi kwenye mashindano ya CAF (Shirikisho la Soka Afrika), msimu ujao," alisema Manara.

Aliwataka viongozi na wadau wote wa soka kufikiria vema kabla ya kutoa ushauri namna ambavyo klabu na taasisi mbalimbali ambazo zina mikataba inayohusiana na ligi hiyo.

Naye Ofisa Mtendaji wa TPLB, Almasi Kasongo, aliliambia gazeti hili bodi hiyo bado haijachukua uamuzi mwingine tofauti na itaendelea kusubiri mwongozo mpya utakaotolewa na serikali baada ya siku 30 za awali kumalizika.

Kasongo alisema TFF haijafanya tathmini yoyote kwa sababu janga la corona linasimamiwa na serikali na hivyo watafuata maelekezo mapya yatakayotolewa hapo baadaye.

"Hatujafanya tathmini yoyote mpaka sasa, tumeiachia serikali, kwa kifupi naweza kusema tunatembelea nyota ya serikali, tutasubiri watakapotoa mwongozo, ndio sisi tutatoa tamko," alisema Kasongo.

Aliongeza hadi jana hakuna klabu yoyote iliyowasilisha mapendekezo yake kuhusu hatima ya Ligi Kuu Bara na ligi nyingine kwa maandishi zaidi ya kusikia kwenye vyombo mbalimbali vya habari.

"Pamoja na mitazamo mbalimbali tunayoisikia, sisi suala hili tunasisitiza tumeliachia mikononi mwa serikali," Kasongo alisisitiza.

Michuano ya Kombe la FA yenyewe ilikuwa imeingia katika hatua ya robo fainali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >